# UQAB
Jarida la




*Toleo 28 - Shaaban 1440 H / Mei 2019 Miladi*


**Vipi Khilafah Itakavyozuia Mgawanyiko wa Kimadhehebu**

**Vipi Khilafah Itakabiliana na Ufisadi wa Kisiasa**

**Nidhamu ya Kuadhibu ya Kiislamu**

**Vipi Khilafah Itazuia Dhuluma za Kisiasa?**

**Talaka ni Halali Hata Kama ni Halali Inayo Chukiwa Zaidi**

**Njia ya Mtume (saw) Kuleta Mageuzi - Halaqa 22**




## Vipi Khilafah Itakavyo Angazia Uraia na Wasiokuwa Waislamu

# Vipi Khilafah Itakavyo Angazia Uraia na Wasiokuwa Waislamu

Mwenyezi Mungu (swt) asema:(وَمَا أَرْسَلْنَاكَ إِلَّا رَحْمَةً لِلْعَالَمِينَ) “Nasi hatukukutuma ila uwe ni Rehema kwa walimwengu wote.” [21:107]

Uislamu ulikuja kama angazo kwa wanadamu wote, bila ya kuzingatia dini, dhehebu, tabaka au jinsia. Ndani ya Khilafah raia wote watafurahia manufaa ya nidhamu ya Kiislamu na ulinzi kamili wa maisha yao, mali yao na heshima yao bila ya ubaguzi.

“Raia wote wa Dola ya Kiislamu wanastahiki kufurahia haki na majukumu ya kiShari’ah.” (Kifungu cha 5 – Katiba Kielelezo ya Khilafah ya Hizb ut Tahrir)

Uislamu unapinga fikra zote za kiaswabia, ambazo zilikuwa ndicho kiini cha kuundwa kwa mataifa ya Kimagharibi. Uislamu unayavuka yote haya kwa sababu yananyima kitambulisho kwa msingi wa mtazamo mpana wa ulimwengu. Mtazamo huu umejengwa juu ya ufahamu kuwa viumbe vyote vimeumbwa na Muumba – Mwenyezi Mungu (swt) – na ni vitiifu kwa kanuni yake ya kimaumbile. Kwa mtazamo wa kijamii Uislamu huwatazama wakaazi wote kama wanadamu kuliko kuwatazama kwa makabila au matabaka yao. Natija yake ni wale wanaoishi katika maeneo ya Kiislamu hutazamwa kama raia, bila ya kujali itikadi, rangi au kabila.

Uraia umejengwa juu ya msingi wa ukaazi kuliko kuzaliwa au ndoa. Wale wote wanaobeba uraia ni raia wa Dola, uchungaji wao na usimamizi wa mambo yao ni jukumu la Dola, pasi na ubaguzi wowote. Hivyo basi watu wote wanaobeba uraia wa Kiislamu wanapaswa kutendewa usawa, pasi na kubaguliwa baina yao ima na mtawala, katika upande wa kuangalia mambo yao na katika upande wa kulinda maisha yao, heshima yao na mali yao, au kadhi katika upande wa usawa na uadilifu.

“**Raia wote wa Dola watatendewa usawa bila ya kuzingatia dini, tabaka, rangi au jambo jengine lolote. Serikali inaharamishwa kubagua miongoni mwa raia wake katika mambo yote, iwe katika utawala au mahakama, au uchungaji wa mambo.**” (Kifungu cha 6 – Katiba Kielelezo ya Khilafah ya Hizb ut Tahrir)

Uraia katika Uislamu umo ndani ya mtu aishiye kwa kudumu ndani ya ardhi za Khilafah bila ya kuzingatia makabila yao au itikadi zao. Sio sharti mtu awe Muislamu na kutabanni vipimo vya Uislamu ndio aweze kuwa raia wa dola. Hili limevuliwa kutoka katika Hadith ifuatayo. Mtume (saw) amesema:

ادْعُهُمْ إِلَى الْإِسْلَامِ فَإِنْ أَجَابُوكَ فَاقْبَلْ مِنْهُمْ، وَكُفَّ عَنْهُمْ، ثُمَّ ادْعُهُمْ إِلَى التَّحَوُّلِ مِنْ دَارِهِمْ إِلَى دَارِ الْمُهَاجِرِينَ، وَأَعْلِمْهُمْ أَنَّهُمْ إِنْ فَعَلُوا ذَلِكَ أَنَّ لَهُمْ مَا لِلْمُهَاجِرِينَ، وَأَنَّ عَلَيْهِمْ مَا عَلَى الْمُهَاجِرِينَ

‘Waite katika Uislamu, na ikiwa watakuitikia wakubalie na ujiepushe kupigana dhidi yao, kisha waite kuhama kutoka katika ardhi yao kuja katika ardhi ya waliohama (Muhajirina), na uwajuze kuwa wakifanya hivyo, watakuwa na haki kama za Muhajirina na juu yao watakuwa na majukumu kama ya Muhajirina.’

Raia wasiokuwa Waislamu wanaoishi chini ya Khilafah huitwa katika Shari’ah, kama dhimmi. Neno “dhimma,” lamaanisha “wajibu wa kutimiza mkataba.” Uislamu umekuja na hukumu kadhaa kuhusiana na watu wa dhimmah, ambazo kwazo ulidhamini haki za uraia kwao na kuwalazimisha juu yao majukumu yake. Uislamu pia ulifafanua kuwa dhimmi afurahiye uadilifu ule ule wanaofurahia Waislamu na kwamba wanapaswa kujifunga kwa hukumu zile zile ambazo Waislamu wanajifunga kwazo. Ama kwa yale wanayofurahia katika uadilifu na usawa, hili limevuliwa kutoka katika amri jumla inayojitokeza katika maneno ya Mwenyezi Mungu (swt):

[وَإِذَا حَكَمْتُم بَيْنَ النَّاسِ أَن تَحْكُمُوا بِالْعَدْلِ]

“Na mnapo hukumu baina ya watu hukumuni kwa uadilifu.” (TMQ 4:58)

Na katika maneno yake (swt):

[وَلاَ يَجْرِمَنَّكُمْ شَنَآنُ قَوْمٍ عَلَى أَلاَّ تَعْدِلُواْ اعْدِلُواْ هُوَ أَقْرَبُ لِلتَّقْوَى]

Wala kuchukiana na watu kusikupelekeeni kutofanya uadilifu. Fanyeni uadilifu. Hivyo ndio kuwa karibu mno na uchamngu” (TMQ 5:8)

Na pia inamulikwa katika maneno ya Mwenyezi Mungu (swt) kuhusiana na kuhukumu baina ya watu wa Kitabu

[وَإِنْ حَكَمْتَ فَاحْكُم بَيْنَهُم بِالْقِسْطِ ]

“Na ukiwahukumu, basi hukumu baina yao kwa uadilifu” (TMQ 5:42).

Dola haitaingilia imani au ibada za dhimmi. Wataruhusiwa kushikamana na sheria zao katika mambo ya ndoa na talaka kwa mujibu wa dini yao. Dola itamteua kadhi miongoni mwa watu wao wenyewe ili kutatua mizozo yao kwa msingi wa dini yao katika mahakama za Dola. Katika mambo yanayo husiana na chakula na mavazi wasiokuwa Waislamu wataamiliwa kwa mujibu wa imani yao na ndani ya upeo wa yale ambayo hukumu za kiShari’ah zinazo yaruhusu. Mambo yote mengine yaliyosalia ya sheria na hukumu, kama vile: utekelezaji wa miamala, adhabu na ushahidi (mahakamani), nidhamu za utawala na uchumi hutabikishwa na Dola

*Endelea Uk..3*



Email: info@uqab.or.ke

juu ya kila mmoja, Muislamu na asiyekuwa Muislamu wote sawa sawa. (Kifungu cha 7, Katiba Kielelezo ya Khilafah ya Hizb ut Tahrir). Adam Metz, mwanahistoria wa Kimagharibi, aliandika kuhusiana na Khilafah katika karne ya 4 Hijria, "… dola ya Kiislamu iliwaruhusu watu wa dini nyenginezo kutumia mahakama zao wenyewe. Tunachojua kuhusu mahakama hizi ni kuwa zilikuwa mahakama za kanisa na viongozi maarufu wa kiroho walikuwa ndio mahakimu wakuu."

Kuna Hadith nyingi zinazo amrisha kuwatendea wema dhimmi na kutowadhuru au kuwachukulia kama raia wa tabaka la pili. Mtume (saw) amesema:

أَلَا مَنْ ظَلَمَ مُعَاهِدًا، أَوِ انْتَقَصَهُ، أَوْ كَلَّفَهُ فَوْقَ طَاقَتِهِ، أَوْ أَخَذَ مِنْهُ شَيْئًا بِغَيْرِ»
«طِيبِ نَفْسٍ، فَأَنَا حَجِيجُهُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ

"Jueni kuwa yeyote atakaye mdhulumu aliyehifadhiwa kwa mkataba, au akamlazimisha zaidi ya uwezo wake, akachukua chochote kutoka kwake bila ya ridhaa ya nafsi yake, basi mimi nitakuwa mtetezi wake Siku ya Kiyama."

Wanazuoni wa kale wa Uislamu pia walifafanua haki za Waislamu kwa dhimmi. Mwanachuoni wa kifiqhi maarufu wa dhehebu la Malik, Shaha al-Deen al-Qarafi ameeleza, "Ni jukumu la Waislamu kwa watu wa dhimmi kuwachunga madhaifu wao, kutimiza mahitaji ya maskini, kuwalisha walio na njaa, kuwapa mavazi, kuwahutubia kwa upole, na hata kuvumilia madhara yao hata kama yanatoka kwa jirani, ingawa Waislamu ndio wenye mkono wa juu. Waislamu pia wawashauri kwa ikhlasi juu ya mambo yao na kuwalinda dhidi ya yeyote anayejaribu kuwadhuru wao au familia zao, kuwaibia mali yao, au kukiuka haki zao."

Mwanahistoria wa Kiingereza T. W. Arnold katika kitabu chake, Kuulingania Uislamu, aliandika kuhusiana na muamala wa wasiokuwa Waislamu walioishi chini ya Khilafah Uthmaniya, "… ingawa wayunani kiidadi walikuwa wengi kuliko Waturuki katika mikoa yote ya Ulaya ya himaya hiyo, uvumilivu wa kidini waliopewa, na ulinzi wa maisha na mali waliofurahia, punde tu yaliwaridhisha kupendelea kutawaliwa na Sultan kuliko kutawaliwa na utawala wowote ule wa kinaswara." Mwandishi wa Kiingereza, H.G. Wells, aliandika yafuatayo katika utekelezwaji wa uadilifu na Khilafah: "Waliasisi tamaduni kuu za uvumilivu adilifu. Waliwashajiisha watu kwa hisia ya ukarimu na uvumilivu, na ni wenye utu na uhalisia. Waliunda jamii ya kiutu ambayo ndani yake ilikuwa ni nadra kuona ukatili na madhila ya kijamii, kinyume na jamii nyenginezo zilizokuja kabla yake."

Dhimmi hufurahia manufaa yale yale ya kiuchumi kama Waislamu. Wanaweza kuwa waajiriwa, kuasisi makampuni, kuwa washirika pamoja na Waislamu na kununua na kuuza bidhaa. Mali zao zinahifadhiwa na endapo watakuwa ni masikini na kushindwa kupata kazi wanastahiki kupata ruzuku za dola kutoka katika Hazina ya Khilafah (Bait ul-Mal).

Wasiokuwa Waislamu wanaruhusiwa kuwa wanachama wa Majlis al-Ummah – kitengo cha dola kinachomhisabu Khalifah na kuwakilisha na kuelezea maoni ya watu kwake. Kama mwanachama wa kitengo hiki, wasiokuwa Waislamu wanaweza kusema malalamishi yao kuhusiana na vitendo vya kidhuluma vinavyofanywa na watawala au utabikishaji mbaya wa hukumu za Kiislamu juu yao au ukosefu wa huduma au mfano wake. (Kifungu cha 105, Katiba Kielelezo ya Khilafah ya Hizb ut Tahrir)-

Kihistoria, dhimmi walipata ufanisi ndani ya ardhi za Khilafah. Mwanahistoria wa Kiingereza mwenye asili ya Kiyahudi Cecil Roth anataja kuwa kuamiliwa kwa Mayahudi mikononi mwa Dola ya Uthmaniya kuliwavutia Mayahudi kote barani Ulaya Magharibi. Ardhi ya Uislamu ikawa ndiyo ardhi ya ufanisi. Madaktari wa Kiyahudi kutoka katika chuo cha Salanca waliajiriwa kumhudumia Sultan na mawaziri (Viziers). Katika maeneo mengi utengezaji vioo na uhunzi zikawa ni ukiritimba kwa Mayahudi, na kwa ujuzi wao wa lugha za kigeni, wakawa ndio washindani wakuu kwa wafanyi biashara wa Veneti.

Kodi ya Kiislamu inayofahamika kimakosa zaidi ni jizya. Baadhi ya wanahistoria wanaonyesha sura ya kirongo kuwa kodi ya jizya ilikuwa juu sana hadi dhimmi walilazimika kusilimu ili kuiepuka. Wengine wanaonyesha viwango vya jizya visokuwa na mashiko kama vile asilimia 50.

Uwajibu wa jizya unavuliwa katika Ayah ya Qur'an ifuatayo. Mwenyezi Mungu (swt) asema:

اتِلُوا الَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ بِاللَّـهِ وَلَا بِالْيَوْمِ الْآخِرِ وَلَا يُحَرِّمُونَ مَا حَرَّمَ اللَّـهُ وَرَسُولُهُ
وَلَا يَدِينُونَ دِينَ الْحَقِّ مِنَ الَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ حَتَّىٰ يُعْطُوا الْجِزْيَةَ عَن يَدٍ وَهُمْ
صَاغِرُونَ

"Piganeni na wasio muamini Mwenyezi Mungu wala Siku ya Mwisho, wala hawaharamishi alivyo haramisha Mwenyezi Mungu na Mtume, wala hawafuati Dini ya Haki miongoni mwa waliopewa Kitabu, mpaka walipe kodi (Jizyah) kwa khiyari yao ilhali wao ni wanyonge (saghiroon)." (TMQ 9:29).

'Unyonge' (sighar) huu uliotajwa katika Ayah hii unamaanisha kuwa dhimmi ni lazima ajisalimishe kwa hukumu za Uislamu. Haimaanishi unyonge wa kimwili.

Kodi ya jizya hutekelezwa kwa dhimmi wote watu wazima, wanamume walio na uwezo wa kulipa. Wanawake na watoto wameepushwa na kulipa kama walivyo masikini wasio na njia za kujikimu kimaisha. Jizya hutekelezwa kwa mujibu wa ufanisi wa dhimmi. Katika zama za 'Umar ibn al-Khattab (ra) aliweka vigawanyo vitatu vya jizya kulingana na ufanisi wa mtu. Viwango vya jizya vya wilaya tofauti tofauti za Khilafah katika zama za 'Umar ibn al-Khattab (ra) vimeonyeshwa hapo chini.

Endelea Uk..4

**YEMEN**[28]

| | Dinars (Gold coin) | Weight of dinar in grams | Grams in gold |
|---|---|---|---|
| Everyone eligible | 1 | 4.25 | 4.25 grams |

**IRAQ**[29]

| | Dirhams (Silver coin) | Weight of dirham in grams | Grams in silver |
|---|---|---|---|
| The rich | 48 | 2.975 | 142.80 |
| The middle class | 24 | 2.975 | 71.4 |
| The worker | 12 | 2.975 | 35.7 |

**EGYPT AND ASH-SHAM**[30]

| | Dinars (Gold coin) | Weight of dinar in grams | Grams in gold |
|---|---|---|---|
| The rich | 4 | 4.25 | 17 grams |
| The middle class | 2 | 4.25 | 8.50 grams |
| The worker | 1 | 4.25 | 4.25 grams |

Ni haramu kwa Khilafah kuwabebesha mzigo mkubwa dhimmi kwa utozaji wa kodi kubwa kwani hili huwasababishia wao madhara. Mtume (saw) amesema,

أَلَا مَنْ ظَلَمَ مُعَاهِدًا، أَوِ انْتَقَصَهُ، أَوْ كَلَّفَهُ فَوْقَ طَاقَتِهِ، أَوْ أَخَذَ مِنْهُ شَيْئًا بِغَيْرِ طِيبِ نَفْسٍ، فَأَنَا حَجِيجُهُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ

“Jueni kuwa yeyote atakaye mdhulumu aliyehifadhiwa kwa mkataba, au akamlazimisha zaidi ya uwezo wake, akachukua chochote kutoka kwake bila ya ridhaa ya nafsi yake, basi mimi nitakuwa mtetezi wake Siku ya Kiyama.”

Umar bin Al Khattab (ra) kama Khalifah aliletewa mali nyingi. Abu Ubayd akasema, ‘Naamini, alisema “Ni ya Jizya” – na yeye (Umar) akasema: “Nadhani ni lazima utakuwa umewatia watu uzito (kwa mali kama hiyo).” Wakasema: “Hapana, Wallahi, hatukukusanya chochote ambacho hakikutolewa kwa khiyari bali ni kwa khiyari yao wenyewe.” Akasema: “Pasina kutumia fimbo na pasina kuwafunga kamba?” Wakasema: “Ndio.” Akasema: Namshukuru Mwenyezi Mungu, ambaye hakujaalia haya kutokea mikononi mwangu au wakati wa utawala wangu.”

“Wakati wa Khilafah ya Umawiyya, dhimmi, Manaswara, Majusi, Mayahudi na Masabi, wote walifurahia kiwango fulani cha uvumilivu ambacho leo hatukioni katika nchi za Kinaswara. Walikuwa huru kufanya ibada za dini zao na makanisa yao na mahekalu yao yalihifadhiwa. Walifurahia uhuru ambapo walikuwa ni wafuasi wa sheria za kidini za wasomi na makadhi.” (Will Durant, mwandishi na mwanahistoria wa Kiamerika, Hadithi ya Hadhara – Umri wa Imani)

**Tsuroyya Amal Yasna**
**Mwanachama wa Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**

# Vipi Khilafah Itakavyozuia Mgawanyiko wa Kimadhehebu



Ni Uislamu, thaqafa yake, historia yake na turathi yake ambazo ndizo viunganishi vya kimaumbile vinavyo wafungamanisha Waislamu kote katika Ulimwengu wa Kiislamu, wawe Sunni au Shia, huku nidhamu ya kisekula ya Kimagharibi iliyo lazimishwa juu yao ikipatiliza ikhtilafu zao kwa malengo ya kisiasa. Imani ya Kiislamu inayo waunganisha ni kubwa zaidi kuliko ikhtilafu fulani za kimadhehebu zilizopo baina ya madhehebu tofauti tofauti. Wote wanakubali misingi ya itikadi ya Kiislamu na Qur'an na Sunnah ndio chimbuko la sharia ya Kiislamu. Mwenyezi Mungu (swt) asema,

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُواْ أَطِيعُواْ اللّهَ وَأَطِيعُواْ الرَّسُولَ وَأُوْلِي الأَمْرِ مِنكُمْ فَإِن تَنَازَعْتُمْ فِي شَيْءٍ فَرُدُّوهُ إِلَى اللّهِ وَالرَّسُولِ إِن كُنتُمْ تُؤْمِنُونَ بِاللّهِ وَالْيَوْمِ الآخِرِ ذَلِكَ خَيْرٌ وَأَحْسَنُ تَأْوِيلاً

"Enyi mlio amini! Mtiini Mwenyezi Mungu na mtiini Mtume na wenye madaraka katika nyinyi. Na mkizozana katika jambo basi lirudisheni kwa Mwenyezi Mungu na Mtume ikiwa mnamuamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho. Hayo ndiyo bora na yenye mwisho mwema." [An-Nisa: 59]

Ni Uislamu na utawala wa Kiislamu pekee ambao unarekodi ya kushuhudiwa ya kuangamiza umadhehebu na ukabila na kuwaunganisha watu wa usuli, makabila na imani tofauti tofauti kuwa Ummah mmoja na dola moja. Kabla ya Uislamu, makabila ya Aws na Khazraj yalipigana vita vingi dhidi ya wao kwa wao, lakini pindi walipoukubali Uislamu, walikuwa ndugu na kwa pamoja walijulikana kama Answar. Mwenyezi Mungu (swt) asema,

وَأَلَّفَ بَيْنَ قُلُوبِهِمْ لَوْ أَنفَقْتَ مَا فِي الأَرْضِ جَمِيعاً مَّا أَلَّفَتْ بَيْنَ قُلُوبِهِمْ وَلَـكِنَّ اللّهَ أَلَّفَ بَيْنَهُمْ إِنَّهُ عَزِيزٌ حَكِيمٌ

"Na akaziunga nyoyo zao (waumini). Na lau wewe ungelitoa vyote viliomo duniani usingeli weza kuziunganisha nyoyo zao, lakini Mwenyezi Mungu ndiye aliye waunganisha. Hakika Yeye ni Mtukufu Mwenye nguvu, Mwenye hekima." [Al-Anfal: 63]

Waislamu Masunni na Mashia nchini Yemen, Iraq na kwengineko waliishi sako kwa bako kwa amani katika mtaa mmoja kwa karne nyingi chini ya utawala wa Kiislamu wa Khilafah. Walioana, waliswali katika msikiti mmoja na kupigana pamoja dhidi ya maadui wa dola.

Khilafah si dola ya Masunni wala Mashia au dola iliyojengwa juu ya Madhhab yoyote. Bali, ni nidhamu ya kisiasa iliyojengwa juu ya Uislamu kwa Waislamu wote na wanadamu wote, bila ya kujali itikadi, kabila wala utaifa.

Kinyume na serikali na nidhamu zisizokuwa za Kiislamu katika ardhi za Waislamu ambazo hupatiliza tofauti zilizoko baina ya watu kwa malengo ya kisiasa, Khilafah hutazama umoja wa kisiasa baina ya raia wote kwa umuhimu mno. Sera zake za ndani humulika njia ya kipekee katika kuwafinyanga watu tofauti tofauti kuwa mujtama mmoja tulivu unao heshimu tofauti za kidini. Wanaunganishwa pamoja ndani ya Khilafah kwa msingi wa uraia, na haki, dori na majukumu yaliyomo. Khilafah pia itang'oa uangiliaji wowote wa wakoloni katika ardhi za Waislamu, ikiwemo utumizi wa taasubi ya kimadhehebu kuugawanya Ummah.

*Endelea Uk..6*

Raia wote wa Khilafah hufurahia haki sawa za uraia – katika siasa, uchumi, elimu, matibabu na nyanja nyenginezo za kimaisha – bila ya kujali itikadi zao, kabila, jinsi au chochote chengine. Hii ni kwa sababu Uislamu una haramisha ubaguzi baina ya watu katika utoaji haki za uraia. Mtume (saw) asema,

**«ثُمَّ ادْعُهُمْ إِلَى التَّحَوُّلِ مِنْ دَارِهِمْ إِلَى دَارِ الْمُهَاجِرِينَ، وَأَخْبِرْهُمْ أَنَّهُمْ إِنْ فَعَلُوا ذَلِكَ فَلَهُمْ مَا لِلْمُهَاجِرِينَ وَعَلَيْهِمْ مَا عَلَى الْمُهَاجِرِينَ»**

"Kisha waite kuhama kutoka katika ardhi yao kuja katika ardhi ya Muhajirin na uwape habari kuwa hakika wakifanya hivyo watakuwa na haki sawa na Muhajirin na juu yao watakuwa na majukumu sawa na Muhajirin."

"Raia wote wa Dola ya Kiislamu wanastahiki kufurahia haki na majukumu ya Kisheria." (Kifungu cha 5 – Kielelezo cha Katiba ya Khilafah cha Hizb ut Tahrir)

Nidhamu ya kisiasa ya Khilafah haikujengwa juu ya uwakilishi kwa misingi ya ukabila, rangi, au madhehebu ambayo yaweza kuchochea mgawanyiko, uhasama na ushindani baina ya sekta tofauti tofauti za mujtama kwa ajili ya rasilimali na mamlaka. Bali Khalifah (kiongozi wa dola) anawajibika Kiislamu kuwa msimamizi juu ya mahitaji na maslahi ya raia wake wote bila ya kujali itikadi zao, kabila wala asili. Hii ina jumuisha kuhakikisha kila raia wa dola – Sunni au Shia, Muislamu au asiyekuwa Muislamu – mahitaji yao msingi ya chakula, mavazi, makao na elimu yanashibishwa, na kiwango chenye hadhi cha maisha pamoja na kudhamini ulinzi wa damu, imani, heshima, na mali zao.

"Raia wote wa Dola wataamiliwa kwa usawa bila ya kujali dini, jinsi, rangi au jambo lolote jengine. Dola ina haramishwa kubagua miongoni mwa raia wake katika mambo yote, iwe katika utawala au mahakama, au uchungaji wa mambo." (Kifungu cha 6 – Kielelezo cha Katiba ya Khilafah cha Hizb ut Tahrir)

Wale watakao chaguliwa kuwa sehemu ya Baraza la Ummah (Majlis al-Ummah) ambacho ni chombo cha ushauri kinachomhisabu Khalifah kuhusiana na majukumu yake kwa watu na kuwakilisha maslahi ya wote katika jamii zao badala ya maslahi ya vikundi maalumu vya watu ndani ya mujtama.

Khilafah haitatabanni sheria katika kadhia za kiimani au za kiibada katika Uislamu isipokuwa zikiwa na athari ya kijamii kama vile Zakah, na itawaacha Waislamu kufuata dhehebu lolote wanaloliona kuwa na nguvu zaidi katika maeneo hayo. Hii ni kwa sababu kutabanni katika mambo kama haya kwaweza kusababisha uzito na bughdha miongoni mwa wale Waislamu walio na ikhtilafu za rai juu ya kadhia hizi, ambayo nidhamu ya Kiislamu ina kusudia kuzuia. Bali Khilafah itatabanni tu juu ya zile kadhia zinazohitajika kwa ajili ya umoja wa kisiasa na uendeshaji imara wa mambo ya dola pekee. Fauka ya hayo, Khalifah huenda akatabanni kutoka katika dhehebu lolote katika mambo ya dola, iwe la Kisunni au la Kishia, kwa msingi wa rai atakayoiona kuwa yenye nguvu zaidi katika Uislamu.

"Khalifah hatabanni huukmu za kiShari'ah kuhusiana na ibada, isipokuwa zinazohusu Zakah na vita (Jihad). Pia, hatabanni fikra yoyote kuhusiana na Itikadi ya Kiislamu." (Kifungu cha 4 – Kielelezo cha Katiba ya Khilafah cha Hizb ut Tahrir)

Nidhamu ya Elimu ya Khilafah itakuza maadili na ufahamu sahihi wa Kiislamu. Itafanya bidii kujenga fungamano imara la udugu wa Kiislamu baina ya wanafunzi wa Kiislamu ili kutibu na kuzuia migawanyiko yoyote baina ya nyoyo za waumini, ikiwemo kufanya bidii kuondoa fahamu zozote kama taasubi ya kimadhehebu, utaifa na ukabila zinazo sababisha mgawanyiko. Pia itajenga miongoni mwa wanafunzi wake, hisia imara ya uchungaji na majukumu kwa wengine, na haki, mahitaji na maslahi yao, ambayo yatahakikisha mshikamano wa mujtama tulivu.

Nidhamu za mahakama na kuadhibu wahalifu zitapambana vikali na wale wanaotaka kueneza taasubi ya kimadhehebu au kuwagawanya Waislamu kwa njia yoyote ile. Dola haitakuwa na uvumilivu hata kidogo kwa aina yoyote ya mgawanyiko wa kimadhehebu au ghasia.

**Dkt. Nazreen Nawaz**
**Mkurugenzi wa Kitengo cha Wanawake Katika Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**

# Vipi Khilafah Itakabiliana na Ufisadi wa Kisiasa



Mwenyezi Mungu (swt) asema,

وَلَوْ اتَّبَعَ الْحَقُّ أَهْوَاءَهُمْ لَفَسَدَتْ السَّمَوَاتُ وَالأَرْضُ وَمَنْ فِيهِنَّ بَلْ أَتَيْنَاهُمْ بِذِكْرِهِمْ فَهُمْ عَنْ ذِكْرِهِمْ مُعْرِضُونَ

"Lau Haki ingalifuata matamanio yao, basi zingeli haribika mbingu na ardhi na waliomo ndani. Bali tumewaletea ukumbusho wao, nao wanajitenga na ukumbusho wao." [Al-Mu'minun: 71]

Hivyo basi, endapo Mwenyezi Mungu atafanya yale ambayo washirikina hawa wanayataka na kusimamia mambo kwa mujibu wa matakwa na matamanio yao na kuachana na haki wanayoichukia, mbingu na ardhi na vilivyomo ndani yake vingefisidika; hii ni kwa sababu hawajui matokeo ya vitu na wema na ufisadi wa usimamizi (tafsiri ya Tabari). Hali ya maisha haya sio sahihi, kutengea kwake kunawezekana pekee kupitia zile hukumu na tiba ambazo Mwenyezi Mungu (swt) amezipitisha ambazo ameziteremsha kwa watu kama uongofu na rehema.

Uislamu ni itikadi ambayo kwayo huchipuza nidhamu inayo waongoza watu katika njia za kheri na mafanikio. Ulikuja kusahihisha ulimwengu na kutawala ulimwengu, na endapo utakosekana maishani mwao, ufisadi utatawala na watu watapotea. Ufisadi humaanisha kukengeuka kutokana na njia ya sawa, kuonyesha uasi kwa Mwenyezi Mungu (swt) juu ardhi na kutojisalimisha kwa Uungu wake (swt):

إِنَّ هَذَا لَهُوَ الْقَصَصُ الْحَقُّ وَمَا مِنْ إِلَهٍ إِلَّا اللَّهُ وَإِنَّ اللَّهَ لَهُوَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ * فَإِنْ تَوَلَّوْا فَإِنَّ اللَّهَ عَلِيمٌ بِالْمُفْسِدِينَ

"Hakika haya ndiyo maelezo ya kweli. Na hakuna mungu isipokuwa Mwenyezi Mungu tu. Na hakika, Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye nguvu, Mwenye hikima. Na kama wakigeuka basi Mwenyezi Mungu anawajua waharibifu." [Al-i-Imran: 62-63].

Kile ambacho Mwenyezi Mungu anakichukulia kuwa ufisadi basi ni hivyo, hata kama baadhi ya watu watakiona vyenginevyo. Mwenyezi Mungu (swt) asema:

وَإِذَا تَوَلَّى سَعَى فِي الْأَرْضِ لِيُفْسِدَ فِيهَا وَيُهْلِكَ الْحَرْثَ وَالنَّسْلَ وَاللَّهُ لَا يُحِبُّ الْفَسَادَ

"Na anapo tawala hufanya juhudi katika nchi kwa kufisidi humo na kuteketeza mimea na viumbe. Na Mwenyezi Mungu hapendi ufisadi." [Al-Baqarah: 205]

Kwa hivyo, kuhukumu kitendo kuwa chema au fisidifu, ni lazima tuwe na kipimo. Kipimo hiki ni lazima kiwe cha Kisheria na sio cha kiakili; kwani endapo kitakuwa cha kiakili, kila mtu atadai kuwa kile anachokifanya ni wema na ilhali ni ufisadi, kama walivyo sema watu wa Firauni:

*Endelea Uk..8*

...أَتَذَرُ مُوسَى وَقَوْمَهُ لِيُفْسِدُوا فِي الْأَرْضِ وَيَذَرَكَ وَآلِهَتَكَ

"Unamuacha Musa na watu wake walete uharibifu katika nchi na wakuache wewe na miungu yako? ..." [Al-A'raf: 127].

Wahemishwa miongoni mwa watu wa Firauni walimuhukumu Musa na watu wake kuwa wafisadi na kutoa hoja kuwa Firauni ndiye mtengezaji … Hukumu hii imejengwa juu ya matamanio na maslahi, ambazo hutoa hukumu ya kimakosa na fisidifu.

Kuiachia akili kuhukumu vitendo kwa wema au ufisadi hakutapelekea katika natija sahihi au hukumu sahihi. Sheria iliyotungwa na akili hukisifu kila kilicho nje ya upeo wake au hukiita chengine kisicho kuwa hicho kuwa fisidifu na chenye kufisidi: hivyo basi, Mrasilimali kwa mujibu wa wakomunisti ni mfisadi na Muislamu kwa mujibu wa warasilimali ni mfisadi … kwa msingi wa fahamu zinazo chipuza kutokana na imani hizi na hutofautiana kwa mujibu wa mfumo.

وَإِذَا قِيلَ لَهُمْ لَا تُفْسِدُوا فِي الْأَرْضِ قَالُوا إِنَّمَا نَحْنُ مُصْلِحُونَ * أَلَا إِنَّهُمْ هُمُ الْمُفْسِدُونَ وَلَكِنْ لَا يَشْعُرُونَ

"Na wanapoambiwa: Msifanye uharibifu ulimwenguni. Husema: Hakika sisi ni watengenezaji. Tambueni! Hakika wao ndio waharibifu lakini hawatambui." [Al-Baqarah: 11-12]

- Ufusadi wa kisiasa (ufisadi katika uchungaji wa mambo ya watu) kwa ujumla ni ufisadi wa nidhamu inayo endesha mambo ya kimaisha ambayo hayawezi kuwa sawa isipokuwa yatawaliwe kupitia nidhamu ya Muumba wake:

وَمَنْ أَعْرَضَ عَن ذِكْرِي فَإِنَّ لَهُ مَعِيشَةً ضَنكاً وَنَحْشُرُهُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ أَعْمَىٰ

"Na atakaye jiepusha na mawaidha yangu, basi kwa yakini atapata maisha yenye dhiki.'" [Ta-Ha: 124]

Ufisadi ni kuachana na sheria ya Mwenyezi Mungu na kutabanni sheria nyengineyo isiyokuwa ya Mwenyezi Mungu. Hivyo basi, Mtume (saw) alikuwa makini kusimamisha utawala wa Mwenyezi Mungu duniani, ili yeye (saw) aeneze ujumbe huu, atekeleze amana na kuweka misingi ya dola inayo linda kheri na kupigana na maadui wake na kusimama wima kwa ajili ya kudumu kwake kupitia kuhasibu na kuzuia kila ufisadi ndani na nje ya Dola hiyo.
Hivyo basi, vipi dola ya Khilafah itapiga vita ufisadi na watu wake?

Kupitia Jihad, Khilafah imeeneza sheria ya Mwenyezi Mungu … na kupitia Jihad, kheri na wema zilitawala … na kupitia kwayo, watu walitolewa kutoka katika giza hadi katika nuru na iliwalingania kumuabudu Mola wa watu na kuachana na kila aina ya ufisadi uliokuwa nyuma yake … Haikulazimisha watu kuingia katika Uislamu, bali ilifanya kazi kuufanya ulimwengu usitawaliwe kwa chengine chochote isipokuwa kheri hii na kuwatabikishia watu sheria zake na uadilifu na rehema zilizomo ndani yake!

Katika upande wa nje, Dola ya Khilafah imeeneza Kheri (Uislamu) kote duniani, hivyo basi eneo lake limepanuka … na ilizuia ufisadi (sheria zilizotungwa na binadamu) hivyo, kuzidunisha na kufanya kazi kuziondoa. Huku kindani, Khilafah ikipigana na ufisadi na wafisadi, na kuzuia udhalimu na madhalimu, na haikumruhusu yeyote kuwatawala Waislamu isipokuwa achaguliwe na Ummah, hivyo, mamlaka yako kwa Ummah na ni Ummah pekee ndio wenye haki ya kumteua yule wanayemuona kustahiki ili kutabikisha sheria ya Mwenyezi Mungu.

Hakuna yeyote anaye lazimishwa kuwa Khalifah kwa Ummah na hairuhusiwi kumlazimisha yeyote kumchagua nani atakaye kuwa Khalifah, hii ni kwa sababu "Khilafah ni mkataba wa khiyari na maridhiano" (Kifungu cha 25 cha Katiba Kielelezo ya Dola ya Khilafah iliyo tayarishwa na Hizb ut Tahrir).

Kila Muislamu ana haki ya kumchagua Khalifah na kumpa ahadi ya utiifu (Bay'ah). Mkataba wa Khilafah hufungwa kwa mtu kupitia bay'ah ya uteuzi ya wale waliochaguliwa na Ummah ili kuuwakilisha katika utoaji bay'ah hiyo ya uteuzi, huku bay'ah ya waliosalia katika watu ikiwa ni bay'ah ya utiifu na sio bay'ah ya uteuzi "yeyote anaye onekana kuwa na uwezo wa kuasi hulazimishwa kutoa bay'ah hiyo" (Kifungu cha 27 cha Katiba Kielelezo).

- Endapo mtu atachukua Khilafah pasi na utiifu wa Ummah basi huyo atakuwa amenyakua haki yake na mamlaka na ameingia hatua ya kwanza katika njia ya ufisadi, na Ummah lazima wasimame dhidi yake, kumzuia na kuyaregesha mamlaka na kumchagua yule wanayemuona kustahiki mamlaka hayo, "Hakuna yeyote atakaye kuwa Khalifah isipokuwa ateuliwe na Waislamu, na hakuna yeyote atakaye miliki mamlaka ya lazima ya uongozi wa Dola hiyo isipokuwa baada ya mkataba naye kukamilishwa kwa mujibu wa Shari'ah, kama ulivyo mkataba wowote katika Uislamu." (Kifungu cha 28 cha Katika Kielelezo).

- Kumhisabu Khalifah ni jukumu juu ya Ummah; "Waislamu kuwahisabu watawala ni moja ya haki zao na wajibu toshelezi juu yao.

Raia wasiokuwa Waislamu wana haki ya kutoa malalamishi yao kuhusiana na dhuluma ya mtawala kwao au utabikishaji wa kimakosa wa hukumu za Kiislamu juu yao." (Kifungu cha 20 cha Katiba Kielelezo ya Dola ya Khilafah iliyo tayarishwa na Hizb ut Tahrir). Mtume (saw) asema:

أَلاَ مَنْ ظَلَمَ مُعَاهِداً، أَوْ انْتَقَصَهُ، أَوْ كَلَّفَهُ فَوْقَ طَاقَتِهِ، أَوْ أَخَذَ مِنْهُ شَيْئاً بِغَيْرِ طِيبِ نَفْسٍ، فَأَنَا حَجِيجُهُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ

"Tambueni, yeyote mwenye kumdhulumu aliye hifadhiwa kwa mkataba, au akamkalifisha juu ya uwezo wake, au akampokonya kitu pasi na ridhaa yake, basi mimi nitakuwa mtetezi wake Siku ya Kiyama." (Imesimuliwa na

***Endelea Uk..9***

Abu Dawood). Hivyo basi, utabikishaji mbaya wa hukmu za Shari'ah huchukuliwa ni kitendo cha dhuluma, na kulalamika juu yake ni haki kwa Muislamu na Dhimmi, kwani Mtume (saw) amesema:

وَإِنِّي لأَرْجُو أَنْ أَلْقَى رَبِّي وَلَيْسَ أَحَدٌ مِنْكُمْ يَطْلُبُنِي بِمَظْلِمَةٍ

"Na hakika mimi nataraji kukutana na Mola wangu na hali hakuna hata mmoja miongoni mwenu atakaye dai kutoka kwangu niliyomdhulumu." (imeripotiwa na Al-Tirmidhi aliye sema riwaya hii ni Hasan Sahih).

مَنْ أَخَذْتُ لَهُ مَالاً فَهَذَا مَالِي فَلْيَأْخُذْ مِنْهُ، وَمَنْ جَلَدْتُ لَهُ ظَهْراً فَهَذَا ظَهْرِي... فَلْيَقْتَصَّ مِنْهُ

"... Yeyote niliyechukua mali yake, basi hii hapa mali yangu; na achukue kutoka kwayo, na yeyote niliyemchapa mjeledi mgongo wake, basi huu hapa mgongo wangu; basi na auchape mjeledi." Hivyo basi, ili kupata utawala wa Mwenyezi Mungu na uadilifu duniani ni wajibu kwa Ummah – baada ya kutoa utiifu wake kwa Khalifah waliyemridhia kuwatawala kwa yale yote yaliyo teremshwa na Mwenyezi Mungu– kumhisabu na kupeleka mambo yake Mahakama ya Madhalim (kupitia Baraza la Ummah) endapo atakataa kujiepusha kutokana na ufisadi wake na mahakama hiyo ina haki ya kumuuzulu.

- Rafiki na Swahaba wa Mtume (saw), Abu Bakr al-Siddiq alisema pindi alipochukua Khilafah kwa Waislamu:

إن أحسنت فأعينوني، وإن أسأت فقوّموني، الصّدق أمانة، والكذب خيانة، والضّعيف فيكم قويّ عندي حتّى أريح عليه حقّه إن شاء الله، والقوىّ فيكم ضعيف حتّى آخذ الحقّ منه إن شاء الله

"Nimetawalishwa juu yenu, ilhali mimi si katika wabora wenu. Nikifanya mazuri, nisaidieni; na nikikosea, ninyoosheni. Ukweli ni amana na urongo ni khiyana. Mnyonge kwenu kwangu mimi ni mwenye nguvu mpaka nimrudishie haki yake kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu, na mwenye nguvu kwenu kwangu ni mnyonge mpaka niichukue haki kutoka kwake kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu."

Hivyo basi, swahaba huyu wa Mtume wa Mwenyezi Mungu aliuelewa ujumbe huu na kwa uongofu wa Mtume wake (saw), alitekeleza amana, na kuomba ushauri wa watu na usaidizi, na kwa njia yake hii Maswahaba na Tab'ieen waliifuata, hivyo walitawala na kunyanyua uadilifu na kueneza rehema na uongofu wa Mwenyezi Mungu.

- Ujumbe wa Uislamu ni Ahkam za kiShari'ah zinazotekelezwa ardhini kwa ajili ya furaha ya wanadamu, na maagizo haya hutekelezwa kwa kupatikana Khalifah. Uwepo wake ni wajib ili kupata wema, na endapo atakosekana, ufisadi hutawala … Lakini Khalifah huyu au wengineo walio na jukumu la kutabikisha Hukumu wanaweza kufanya makosa – kwa kuwa wao ni binadamu – hivyo Uislamu umeweka vidhibiti ili kutotoa mwanya kwa dhuluma na kuenea kwa ufisadi … Katika Seera ya Mtume wetu kipenzi chetu kuna mafunzo bora, kwani yeye alijifunga na sheria ya Mola wake na hakukengeuka kutokana nayo … Alisimamisha adhabu za kisheria (Hudud), pasi na kulegeza msimamo au kubagua raia wake … Aliapa kwa Allah akisema:

وَايْمُ اللَّهِ لَوْ أَنَّ فَاطِمَةَ بِنْتَ مُحَمَّدٍ سَرَقَتْ لَقَطَعْتُ يَدَهَا

"Naapa kwa Mwenyezi Mungu lau Fatimah binti Muhammad ataiba nitaukata mkono wake." Ikidhihirisha fikra safi na wazi ambayo yeye (saw) aliifuata na kwa hivyo akaongoka na kwayo akawaongoza wale waliomuamini Mwenyezi Mungu kama Mola wao na Muhammad kama Nabii na Mtume wao. Maswahaba na Tabi'een walimfuata katika hilo na wakafuata njia yake. Hivyo basi, Umar (r.a) alitekeleza adhabu ya kisheria ya unywaji (vilevi) juu ya mtoto wake kwa sababu alijua kuwa alikunywa aina fulani ya kinywaji ambacho kinalewesha.

- Omar bin al-Khattab (ra) amesema:

أرأيتم إن استعملت عليكم خير ما أعلم ثم أمرته بالعدل فيكم، أكنت قضيت ما علي؟ قالوا: نعم، قال: لا، حتى أنظر في عمله أعَمِل بما أمرته أم لا

"Mwaonaje lau nitamteua juu yenu mbora kati ya wale ninaowajua kisha nikamwamrisha kuwa mwadilifu kwenu, je, nitakuwa nimetimiza yale yaliyo juu yangu?" Wakasema: ndio. Akasema: "Hapana, hadi niangalie katika matendo yake – je, ametenda kwa yale niliyo mwamrisha au la." Ingawa uangalizi wa Muislamu binafsi unaanza kwa kujitazama binafsi kunakotekelezwa na Muislamu mwenyewe, licha ya hivyo mwanadamu, ni mkosefu na ni watu wachache wanaoweza kukaa mbali na mtelezo huu.

Hivyo basi, matendo ya mtu yanahitaji kuangaliwa, na Mwenyezi Mungu amelifanya jukumu la uangalizi kuwa jukumu jumla la dola na jamii nzima ya Waislamu. "Ni wajib kwa Khilafah kuchunguza vitendo vya wasaidizi waliowekwa (Tafwidh) na usimamizi wao wa mambo, ili kuthibitisha kile kilicho sahihi, na kurekebisha makosa yoyote, kwani usimamizi wa mambo ya Ummah umewakilishiwa Khalifah na huamuliwa kupitia ijtihad yake" (Kifungu cha 46 cha Kielelezo cha Katiba ya Dola ya Khilafah). "Khalifah ni lazima achunguze vitendo vya magavana na kutathmini kwa kuendelea utendakazi wao kwa umakinifu. Ni lazima awape niaba watu kuangalia hali zao, kuwachunguza, na mara kwa mara kuwakusanya wote au baadhi yao, na kusikiza malalamishi ya raia kuwahusu" (Kifungu cha 60 cha Kielelezo cha Katiba ya Dola ya Khilafah). Watangulizi (Salaf) wa Ummah walifuata mwelekeo huu ili kung'oa ufisadi kutoka katika jamii ya Kiislamu na kuondoa alama zake.

Hivyo basi, tatizo sio uwepo wa watu wafisadi ndani ya dola, bali tatizo ni kujitia upofu juu ya ufisadi na kutowaadhibu wafisadi, wanaofisidi. Kuna mwanya mkubwa kati ya mtawala mwadilifu anayepigana na ufisadi na kumuomba Mwenyezi Mungu (swt) kumpa

*Endelea Uk..10*

mafanikio ili kutabikisha hukumu zake, na mtawala mfisadi anaye kwepa na kuasi, bali, anapiga mahesabu pamoja na watu wafisadi na kuamiliana nao, na hivyo basi kumkhini Mwenyezi Mungu na Mtume wake na waumini, na atapokea kutoka Mwenyezi Mungu kile anachostahiki.

- Katika "utawala wa kidemokrasia" watu wafisadi huhalalisha ufisadi wao, na ndani ya demokrasia hupitisha kanuni zinazotumikia maslahi yao na kuidhinisha maovu yao. Ili kupata hili, tunawaona wakitilia nguvu kampeni zao za uchaguzi, wakiwasiliana na watu na kutumia pesa ili kuhakikisha idadi ya juu zaidi ya kura, na baadaye, baada ya kuwatawala kwa "demokrasia" yao wanageuka na kukusanya viwango vikubwa vya pesa ili kufidia zile walizotumia maradufu. Huku tukiona kuwa chini ya sheria ya Mwenyezi Mungu amana hii haipewi wale wanaoitafuta, kwa hofu kuwa huenda akapotoka na kudanganywa kuhusu Mwenyezi Mungu na mdanganyaji, na hivyo kupotea, kuwa mfisadi na kutenda ufisadi. Mtume (saw) amesema:

إنَّا وَاللَّهِ لا نُوَلِّي عَلَى هَذَا الْعَمَلِ أَحَدًا سَأَلَهُ، وَلا أَحَدًا حَرَصَ عَلَيْهِ

"Hakika sisi kwa Jina la Mwenyezi Mungu hatumteui yeyote kwa kazi hii anaye itafuta, wala yeyote anayeigombania."

Yeyote anayetafuta wadhifa wa Khilafah na kuuomba na kuugombania anautafuta kwa ajili ya nafsi yake, na ana matarajio na manufaa ya kibinafsi, na yeyote aliye hivyo kamwe hata tafuta maslahi ya wengine na hatakuwa na hamu ya kuwanufaisha. Hivyo, Abu Dharr alipouomba, na yeye ni mwema na mwaminifu, akisema:

يَا رَسُولَ اللَّهِ أَلَا تَسْتَعْمِلُنِي؟

قَالَ:

فَضَرَبَ بِيَدِهِ عَلَى مَنْكِبِي ثُمَّ قَالَ: يَا أَبَا ذَرٍّ إِنَّكَ ضَعِيفٌ وَإِنَّهَا أَمَانَةُ وَإِنَّهَا يَوْمَ الْقِيَامَةِ خِزْيٌ وَنَدَامَةٌ إِلَّا مَنْ أَخَذَهَا بِحَقِّهَا وَأَدَّى الَّذِي عَلَيْهِ فِيهَا

"Nilisema: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, mbona usiniteue (kwa wadhifa rasmi)? Akanipiga kwa mkono wake juu ya bega langu kisha akasema: "Ewe Abu Dharr hakika wewe ni dhaifu na hakika hii ni amana na hakika hii itakuwa ndio sababu ya fedheha na majuto siku ya Kiyama isipokuwa kwa atakayeibeba kwa haki yake na kutimiza yale aliyoteuliwa kwayo (kutekeleza majukumu yake ipaswavyo)"

Ufisadi wa kisiasa ambao umeukumbuka Ummah wa Kiislamu na ulimwengu kwa jumla chini ya demokrasia hii iliyooza, pamoja na sheria zake dhalimu, hauwezi kumalizwa na hauwezi kuondolewa isipokuwa kwa kupitia nidhamu ya utawala ya Kiislamu, "Khilafah kwa njia ya Utume". Ndiyo pekee itakayo pambana na ufisadi, kwa sababu sheria zake huidhinishwa kwa mujibu wa maagizo ya Mwenyezi Mungu (swt), sio kwa mujibu wa matamanio na mapendeleo ya watawala wanaochimba mahandaki baina yao na Ummah, ambao hawaaminiwi kwa Dini ya Mwenyezi Mungu wala kwa maisha ya watu, na ambao wananufaishwa na makafiri katika kueneza ufisadi na kuuzuia Ummah kutokana na kushikamana na Uislamu na kutabanni hukumu zake na kuishi chini yake.

Ili kuondoa ufisadi … na kuwaregeshea watu usalama, utulivu na ufanisi … ni wajibu kwa Waislamu kujiunga na kazi ya kuregesha maisha kamili ya Kiislamu na kuishi chini ya hukumu adilifu za Mola wao, na kufanya bidii ili kuondoa demokrasia na ufisadi wake na mateso ya wanadamu hadi ahadi ya Mwenyezi Mungu ipatikane:

وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنْكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَى لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُمْ مِنْ بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْناً يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئاً وَمَنْ كَفَرَ بَعْدَ ذَلِكَ فَأُولَئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ

"Mwenyezi Mungu amewaahidi wale walioamini miongoni mwenu na kutenda mema atawafanya makhalifah katika ardhi kama alivyo wafanya makhalifah wa kabla yao, na kwa yakini atawasimamishia Dini yao aliyowapendelea, na atawabadilishia amani baada ya khofu yao, Wawe wananiabudu Mimi, wala wasinishirikishe na chochote. Na watakao kufuru baada ya hayo, basi hao ndio wapotovu." [An-Nur: 55].

Na bishara ya Mtume (saw) isimame:

ثُمَّ تَكُونُ مُلْكاً جَبْرِيَّةً فَتَكُونُ مَا شَاءَ اللَّهُ أَنْ تَكُونَ ثُمَّ يَرْفَعُهَا إِذَا شَاءَ أَنْ يَرْفَعَهَا... ثُمَّ تَكُونُ خِلَافَةٌ عَلَى مِنْهَاجِ النُّبُوَّةِ ثُمَّ سَكَتَ

"... kisha utakuwepo utawala wa mabavu, na utakuwepo kwa muda apendao Mwenyezi Mungu uwepo kisha atauondoa apendapo kuuondoa, kisha itakuwepo Khilafah kwa njia ya Utume, kisha (saw) akanyamaza". (Imesimuliwa na Ahmad).

**Imeandikwa kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na**

**Zainah As-Saamit**

# Nidhamu ya Kuadhibu ya Kiislamu

Ni baraka za Mwenyezi Mungu (swt) kumtuma Mtume wake na Dini ya Haki (Uislamu) na kutubariki sisi na Khilafah ambayo kupitia kwake Ummah wa Waislamu wanabeba jukumu la kulingania ujumbe wa Uislamu kwa wanadamu. Uislamu sio tu dini bali ni nidhamu kamili inayosimamia kila nyanja ya maisha yetu – ima ni akhlaqi au vitendo vya ibada au ni siasa, uchumi au masuala ya kijamii au ni masuala yanayohusiana na sera ya kigeni au nidhamu ya elimu – Uislamu una ahkaam (maamrisho na makatazo) ambayo yanatupa muongozo kamilifu juu ya masuala yote. Mwenyezi Mungu (swt) asema:

وَأَنزَلْنَا إِلَيْكَ الْكِتَابَ بِالْحَقِّ مُصَدِّقًا لِّمَا بَيْنَ يَدَيْهِ مِنَ الْكِتَابِ وَمُهَيْمِنًا عَلَيْهِ فَاحْكُم بَيْنَهُم بِمَا أَنزَلَ اللّهُ وَلاَ تَتَّبِعْ أَهْوَاءهُمْ عَمَّا جَاءكَ مِنَ الْحَقِّ لِكُلٍّ جَعَلْنَا مِنكُمْ شِرْعَةً وَمِنْهَاجًا

"Na tumekuteremshia wewe, kwa haki, Kitabu hichi kinacho sadikisha yaliyo kuwa kabla yake katika Vitabu na kuyalinda. Basi hukumu kwa aliyo yateremsha Mwenyezi Mungu, wala usifuate matamanio yao ukaacha Haki iliyo kujia. Kila mmoja katika nyinyi tumemwekea sharia yake na njia yake." (TMQ 5:48) Hivyo basi, Shari'ah ambazo zilizomshukia Mtume wetu (saw) kwa njia ya Qur'an na Sunnah zimejumuisha ndani yake ahkaam kuhusiana na mahakama, uhalifu, viapo, ushahidi na adhabu ambazo zinatekelezwa na Dola ya Kiislamu.

Kwa miaka 1300, Khilafah ilikuwa ikiwatekelezea haki raia wake kwa kuwatekelezea sheria hizo mfano katika eneo la India lilikuwa likisimamiwa na sheria za Kiislamu mpaka Waingereza walipowasili na kuzifutilia mbali. Tokea wakati huo mizozo baina ya watu ina hukumiwa kwa Ukafiri (sheria ambazo sio za Kiislamu). Baada ya kupata uhuru kutoka kwa wakoloni Waingereza, Waislamu walitakiwa watekeleze sheria za Kiislamu kuhusiana na adhabu. Lakini, uongozi wa kisiasa wa Pakistan ulijisalimisha kwa utawala wa kifikra wa Kimagharibi na kuchukua sheria za Uingereza zikiwa na tofauti ndogo, hivyo kuyatelekeza maamrisho ya Mwenyezi Mungu (swt).

وَمَن لَّمْ يَحْكُم بِمَا أَنزَلَ اللّهُ فَأُوْلَـئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ

"Na wasio hukumu kwa yale aliyo yateremsha Mwenyezi Mungu basi hao ndio wapotofu." [TMQ 5:47] Kuzidi kwa viwango vya uhalifu leo nchini Pakistan ni kutokana na kutotekelezwa kwa hukumu za nidhamu ya adhabu ya Kiislamu.

Ili kulemaza hisia za Waislamu, adhabu chache za Kiislamu zimetekelezwa na pia zikiwa hazina ikhlass ndani yake kama inavyoshuhudiwa katika utekelezwaji wake ambapo muundo wa mahakama, sheria za viapo, ushahidi na utambulishwaji wa uhalifu zimekitwa kwa mujibu wa fikra za Ukafiri. Hivyo basi, rai ya eti "Hukumu za Kiislamu" hazikuacha athari yoyote muhimu katika maisha ya Waislamu.

Miongo ya muendelezo wa utekelezaji wa sheria za Ukafiri zimeziba sura ya mahakama na nidhamu ya adhabu ya Uislamu katika akili za Waislamu leo. Zaidi ya hayo, athari ya thaqafa ya Kimagharibi kutokana na kupigiwa debe na wakoloni imeteka akili za Waislamu kiasi kwamba imefikia kuuliza baadhi ya masuali kwa sheria za Kiislamu. Lengo la Makala hii ni kuonyesha namna nidhamu ya adhabu ya Uislamu ilivyo. Mwenyezi Mungu (swt) awaongoze Waislamu kuweza kutekeleza Shari'ah ya Muhammad (saw) kwa ukamilifu kupitia kusimamisha tena Khilafah na Yeye (swt) atubariki tuwe na mujtama wa Kiislamu ambapo uhalifu utakuwa mchache kiasi kwamba ni vigumu kuusikia.

Aina za Adhabu (Uqoobah)

Kuna aina nne za adhabu za kiShari'ah:

1. Hudood (adhabu ambazo zimekatika)
2. Jinayaat (adhabu za uhalifu)
3. Ta'zeer (adhabu ambazo hazijakatika)
4. Mukhalafaat (adhabu za kwenda kinyume)

**Maana ya uhalifu kiShari'ah**

Kabla kuingia kina katika kila aina ya adhabu, ni muhimu kuelewa maana ya uhalifu kwa mujibu wa Shari'ah. Hukumu za kiShari'ah zinazohusiana na vitendo vya mwanadamu ni tano: faradhi (lazima), mandub (imependekezwa), mubah (imeruhusiwa), haramu (imekatazwa) na makruh (haipendezi). Faradhi ni amrisho la lazima kufanywa na ukiliacha wapata dhambi, mandub ni amrisho ambalo ukilifanya wapata thawabu na usipolifanya hupati dhambi, mubah ni amrisho ambalo ukilifanya hupati thawabu na usipolifanya hupati dhambi, haramu ni amrisho ambalo ukilifanya wapata dhambi na makruh ni amrisho ambalo ukilifanya hupati dhambi na ukiliwacha wapata thawabu.

Vitendo ambavyo adhabu zimewekwa juu yake ni vile vya kutelekeza faradhi, kutenda haramu na kwenda kinyume na maagizo ya Serikali ya Kiislamu. Kosa (uhalifu) ni kitendo baya (qabeeh) ambacho Shari'ah imekifanya ni kosa; ima kitendo hicho kiwe kinaingia chini ya haramu (kimekatazwa) au Shari'ah imeweka adhabu maalum kwa kitendo hicho. Hivyo basi, vitendo haviwi uhalifu ikiwa Shari'ah haijasema hivyo. Hivyo basi, kiujumla hakuna adhabu juu ya vitendo vya makruh na mubah. Lakini, Shari'ah imempa Khalifah haki ya kutoa maagizo ya adhabu kwa ukiukaji baadhi unaoingia

*Endelea Uk..12*

katika Mukhalafaat mfano ukiukaji kuhusiana idara ya Serikali ya Kiislamu, ujenzi wa majengo na sheria za barabarani n.k. Zaidi ya hayo, hakuna adhabu kutokana na kutelekeza mandub au kufanya kitendo cha makruh kwa sababu Mwenyezi Mungu (swt) ana adhibu tu kwa kutotenda faradhi na kutenda haramu.

Hivyo basi, vitendo vyote ambavyo vimejumuishwa katika uhalifu ima vinatokamana na maarisho na makatazo au vinatokamana na tabbani ya Khalifah kwa mujibu wa ijtihad na ndio vilivyo na adhabu chini ya nidhamu ya adhabu ya Kiislamu.

Kwa nini kuweko na sheria za kuadhibu?

Kutenda uhalifu hakupo ndani ya maumbile ya mwanadamu. Na pia sio maradhi ambayo yamemuathiri mwanadamu. Bali ni kukiuka nidhamu ambayo imempangia mwanadamu vitendo vyake.

Mwenyezi Mungu (swt) alimuumba mwanadamu na akaumba ghariza na mahitaji ya kiviungo ndani ya mwanadamu. Ghariza na mahitaji ya kiviungo ni nishati muhimu ndani ya mwanadamu ambayo humpelekea kushibisha. Kwa hivyo mwanadmu hutenda vitendo vyake ili kuweza kushibisha. Kuacha kushibisha ghariza na mahitaji ya kiviungo pasina nidhamu husababisha vurugu. Hivyo basi, ili kupangilia vitendo vya mwanadamu, Mwenyezi Mungu (swt) akateremsha ahkaam al-Shari'ah (sheria za Kiislamu) ambazo zinatupa muongozo kamilifu juu ya vitendo vyetu. Mwenyezi Mungu (swt) aliweka hukumu katika halali (zimeruhusiwa) na haramu (zimekatazwa). Mwenyezi Mungu (swt) alimhutubia mwanadamu kufanya vitendo ambavyo ni faradhi au kujiepusha na vitendo vya haramu. Hivyo basi, yule anaye telekeza faradhi au anaye tenda haramu amefanya kitendo kibaya (qabeeh) na hivyo kustahiki kuadhibiwa.

Kwa kukosekana adhabu, mujtama hauwezi kuhifadhika na maovu kama alivyosema Mwenyezi Mungu (swt) (وَلَكُمْ فِي ٱلْقِصَاصِ حَيَوٰةٌ) "Mtakuwa nao uhai mzuri katika kulipiza kisasi." (TMQ 2:179). Mwenyezi Mungu (swt) ameelezea kuhusu kulipiza kisasi kwamba ni kitu kinacho okoa maisha katika mujtama. Hili sio kwa kuokoa maisha ya yule aliyeadhibiwa kwa kuwa kulipiza kisasi adhabu yake ni kifo na sio uhai wake, bali kwa yule anayeshuhudia kufanyika kwa kisasi katika mujtama. Mtu mwenye akili anajua kuwa atauliwa ikiwa ataua mwengine. Hivyo basi, ina mkanya asifanye kosa la kuua na hivyo kuulinda mujtama.

Zaidi ya hayo, adhabu itakayo tekelezwa na Dola, hapa duniani kwa mujibu wa dhambi maalum basi itaondosha adhabu akhera, kwani yule ambaye alipewa adhabu ataomba msamaha kwa Mwenyezi Mungu (swt). Mtume (saw) alisema,

وَمَنْ أَصَابَ مِنْ ذَلِكَ شَيْئًا، فَعُوقِبَ فِي الدُّنْيَا، فَهُوَ كَفَّارَةٌ لَهُ. وَمَنْ أَصَابَ مِنْ ذَلِكَ شَيْئًا، ثُمَّ سَتَرَهُ اللَّهُ، فَهُوَ إِلَى اللَّهِ، إِنْ شَاءَ عَفَا عَنْهُ، وَإِنْ شَاءَ عَاقَبَهُ

"Yeyote anayetenda kitendo cha dhambi na akapewa adhabu ya kiShari'ah kuhusiana na hilo, itahesabiwa ni kafara ya dhambi hilo, na yeyote anayetenda dhambi lakini Mwenyezi Mungu akalificha, basi itakuwa ni kwa Mwenyezi Mungu ima amsamehe au amuadhibu." Na Mwenyezi Mungu (swt) amesema,

(قُلْ يَا عِبَادِيَ الَّذِينَ أَسْرَفُوا عَلَى أَنفُسِهِمْ لَا تَقْنَطُوا مِن رَّحْمَةِ اللَّهِ إِنَّ اللَّهَ يَغْفِرُ الذُّنُوبَ جَمِيعًا إِنَّهُ هُوَ الْغَفُورُ الرَّحِيمُ)

"Sema: Enyi waja wangu walio jidhulumu nafsi zao! Msikate tamaa na rehema ya Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu husamehe dhambi zote. Hakika Yeye ni Mwenye Kusamehe, Mwenye Kurehemu." [TMQ 39:53]

Katika historia ya Kiislamu hususan wakati wa Dola ya Kiislamu ya Madina, tunaona kwamba wale waliofanya zinaa walijiwasilisha kwa hiyari yao wenyewe mbele ya Mtume (saw) na baada ya mchakato maalum, yeye (saw) akatangaza hadd (adhabu) juu yao. Hivyo basi, ili kumridhisha Mola wao (swt) na kupata huruma Yake, watu aina hiyo walijisalimisha wenyewe ili waweze kuokolewa na Moto kwa gharama ya adhabu ya duniani.

Hivyo basi, tunapata mazingatio au manufaa kutoka kwa adhabu kwa ujumla. Kwanza, adhabu ni kinga kwani zinawakinga watu kutokana na kufanya uhalifu. Hivyo basi, uhai, mali na heshima zinalindwa kwa kuwa mujtama umekingwa na uhalifu kwa kujifunga kikamilifu kwa kutekeleza adhabu kwa njia ambayo hakuna hata mmoja atakaye fikiria kufanya kosa lolote. Pili, adhabu zinaondosha adhabu za akhera kwa kuwa mtu atamuomba Mwenyezi Mungu (swt) msamaha kama ilivyo elezewa hapo juu.

Nani aliye na mamlaka ya kutekeleza Uqoobaat (adhabu)?

Mamlaka ya kutekeleza adhabu za kiShari'ah yako kwa Khalifah (au Imamu) ambaye anatekeleza adhabu hizo kupitia maagizo ya Dola. Hakuna mtu au shirika ambalo lina haki au jukumu la kutekeleza adhabu kwa watu. Kwa sababu Khalifah anapata mamlaka yake kutoka kwa Ummah kupitia bay'ah (ahadi ya utiifu) na Ummah nao unampa bay'ah kwa sharti kwamba atatekeleza sheria za Kiislamu ndani ya Dola. Kinyume na makundi au mashirika kwani hayana bay'ah kutoka kwa Ummah ili ziwahukumu wala hayatambuliwi kama "Ulil Amr" (wale walio na mamlaka).
Hivyo basi, Khalifah anasimamia mambo ya watu, ana tabbani hukumu za kiShari'ah katika utekelezwaji ndani ya Dola ya Kiislamu na kuwaadhibu wale wanao kiuka sheria hizo.

Mtume (saw) alisema, «الإِمَامُ رَاعٍ وَمَسْؤولٌ عَنْ رَعِيَّتِهِ» "Imamu (Khaleefah) ni mchungaji (ana majukumu) kwa watu aliopewa mamlaka juu yao."

Aina za adhabu za Kiislamu na maelezo yao kwa kifupi

*Endelea Uk..13*

Adhabu za kiShari'ah zimegawanyika aina nne, kama ifuatavyo:

1. Hudood

Shari'ah imeelezea kuwa Hudood ni adhabu zilizopo kwa mujibu wa vitendo vya kihalifu (haramu). Kuadhibiwa kwake ni haki ya Mwenyezi Mungu (swt) na sio wanadamu au Dola. Hivyo basi, adhabu hizo zimetajwa waziwazi katika kitabu, na mtawala au anaye tawaliwa hana haki ya kupunguza au kuondosha adhabu hiyo kwa niaba ya Mwenyezi Mungu (swt). Zinaitwa Hudood, kwa sababu kwa ujumla zinamkinga mwenye kutenda dhambi asirudie kulitenda dhambi hilo ambalo ameadhibiwa kwa hadd (adhabu). Kwa mfano, Mwenyezi Mungu (swt) ameagiza,

الزَّانِيَةُ وَالزَّانِي فَاجْلِدُوا كُلَّ وَاحِدٍ مِنْهُمَا مِائَةَ جَلْدَةٍ وَلاَ تَأْخُذْكُمْ بِهِمَا رَأْفَةٌ فِي دِينِ اللَّهِ

"Mzinifu mwanamke (ambaye hajaolewa) au mwanamume (ambaye hajaoa) mtandikeni kila mmoja katika wao bakora mia. Wala isikushikeni huruma kwa ajili yao katika hukumu ya Mwenyezi Mungu" (TMQ 24:2) na

وَٱلسَّارِقُ وَٱلسَّارِقَةُ فَٱقْطَعُوٓا أَيْدِيَهُمَا جَزَآءًۢ بِمَا كَسَبَا نَكَٰلًا مِّنَ ٱللَّهِ

"Na mwizi mwanamume na mwizi mwanamke, ikateni mikono yao, hayo ni malipo ya waliyo yachuma, ndiyo adhabu ya mfano itokayo kwa Mwenyezi Mungu." (TMQ 5:38).

Hivyo basi, hudood ni adhabu zilizo katika kutoka kwa Mwenyezi Mungu (swt) ambazo zinatekelezwa na mamlaka ya Dola ya Kiislamu.

Kwa mtizamo huu, kuna hadith maarufu ya Rasulullah (saw)

وَالَّذِي نَفْسِي بِيَدِهِ لَوْ كَانَتْ فَاطِمَة بِنْت مُحَمَّدٍ، لَقَطَعْت يَدَهَا

"Naapa kwa Yule ambaye Mkono Wake imo roho yangu! Lau Fatima (binti ya Mtume (saw)) angelifanya hili (angeiba), ningelimkata mkono wake." (Sahih Bukhari 6787).

Hivyo basi, kwa mujibu wa riwaya sahihi haina shaka kuwa hakuna aliye na mamlaka ya kumsamehe mtu ambaye amehukumiwa hadd kwa kosa la kiuhalifu. Hii ni kwa sababu Mwenyezi Mungu (swt) hakutaja kuhusu kafara ya uhalifu. Lakini, lau mtu aliyefanya dhambi akatubia kwa ikhlass na akaadhibiwa kwa hadd basi hapo ndipo atakapo samehewa akhera.

Mwenyezi Mungu (swt) ametufahamisha sisi,

قُلْ يَاعِبَادِي الَّذِينَ أَسْرَفُوا عَلَى أَنْفُسِهِمْ لاَ تَقْنَطُوا مِنْ رَحْمَةِ اللَّهِ إِنَّ اللَّهَ يَغْفِرُ الذُّنُوبَ جَمِيعًا إِنَّهُ هُوَ الْغَفُورُ الرَّحِيمُ

"Sema: Enyi waja wangu walio jidhulumu nafsi zao! Msikate tamaa na rehema ya Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu husamehe dhambi zote. Hakika Yeye ni Mwenye Kusamehe, Mwenye Kurehemu." [TMQ 39:53]

Hivyo basi, uhalifu kama sariqa (uwizi), zinaa, liwat (ngono ya jinsia moja), kunywa khimr (pombe), irtidaad (kuritadi), qadhf (shutuma za zinaa), qutaa' al-turooq (uwizi wa barabara kuu) na uasi unaingia katika hudood ambazo lazima zitekelezwe na Dola ya Kiislamu na ambazo hazina kafara duniani.

2. Jinayaat

Ama kuhusu jinayaat (makosa ya kihalifu) Shari'ah imejumuisha adhabu baadhi katika kikundi hichi. Adhabu hizi zinapewa wale waliotekeleza uhalifu (vitendo vya haramu) ambavyo kuadhibiwa kwake ni haki ya binadamu. Kwa hivyo, mtu ambaye haki yake imekosewa kwa sasabu ya uhalifu ana wezeshwa na Shari'ah ima kulipiza kwa kutaka adhabu au kumsamehe muhalifu kwa mujibu wa hukumu za Kiislamu. Kuua mwanadamu pasina na hatia au kumdhuru kimwili ni makosa ya jinai yanayoadhibiwa kwa mujibu wa Shari'ah. Mwenyezi Mungu (swt) ameagiza:

كُتِبَ عَلَيْكُمُ ٱلْقِصَاصُ فِى ٱلْقَتْلَى ٱلْحُرُّ بِٱلْحُرِّ وَٱلْعَبْدُ بِٱلْعَبْدِ وَٱلْأُنثَىٰ بِٱلْأُنثَىٰ

"Mmepewa ruhusa kulipa kisasi katika walio uwawa-muungwana kwa muungwana, mtumwa kwa mtumwa, mwanamke kwa mwanamke." (TMQ 2:178).

Lakini, lau warithi wa kiShari'ah wa mtu aliyedhuriwa wanataka kumsamehe mkosaji, basi wanaruhusiwa kufanya hivyo kwa kutaka diyyah (pesa za damu) kutoka kwa mtu aliyetenda uhalifu kama alivyotufahamisha Mwenyezi Mungu (swt),

(فَمَنْ عُفِىَ لَهُۥ مِنْ أَخِيهِ شَىْءٌ فَٱتِّبَاعٌۢ بِٱلْمَعْرُوفِ وَأَدَآءٌ إِلَيْهِ بِإِحْسَٰنٍ

"Na anaye samehewa na ndugu yake chochote basi ashikwe kulipa kwa wema, na yeye alipe kwa ihsani." (TMQ 2:178).

Rasulullah (saw) alisema,

مَنْ قُتِلَ لَهُ قَتِيلٌ فَهُوَ بِخَيْرِ النَّظَرَيْنِ إِمَّا أَنْ يَقْتُلَ وَإِمَّا أَنْ يُفْدَى

"Lau mtu ndugu yake ameuliwa, anaweza kuchagua mambo mawili: Anaweza kuchagua muuaji auliwe, au anaweza kutaka pesa za damu." (Sunan Ibn Majah 2624).

Mfano wa uhalifu unaostahiki adhabu au pesa za damu zinajumuisha kuua kimakusudi, kuua bila kukusudia, kudhuru mwili n.k.

3. Ta'zeer

Ta'zeer ni adhabu ambazo hazijakatika na hupewa mtu kutokana na dhambi ambalo halina hadd (adhabu za kukatika) ndani ya Qur'an na Sunnah. Lau muhalifu atapewa adhabu inayostahiki hadd au jinayaat, basi huadhibiwa kwa adhabu maalum na hahukumiwi na

Endelea Uk..14

aina yoyote ya ta'zeer. Lakini, ikiwa Qur'an na Sunnah haikubainisha waziwazi kwa kutaja adhabu kwa kitendo cha uhalifu, basi makosa hayo huadhibiwa kwa ta'zeer. Hivyo basi, ta'zeer ni adhabu kwa madhambi ambayo hakuna hadd au kafara yoyote. Kwa mfano, Shari'ah imeweka adhabu maalum kwa madhara ya kimwili; kwa hivyo uhalifu aina hiyo hautapelekea katika hukumu ya ta'zeer. Zaidi ya hayo, Qadhi (hakimu) atatekeleza hukumu ya ta'zeer kwa mujibu wa hali ya uhalifu uliotekelezwa kwa msingi wa ijtihad (kuelewa waqiah na kuvua hukumu ya kiShari'ah kutokana na ushahidi wa vyanzo vya kiShari'ah). Lakini, Qadhi au Khalifah hawezi kutabbani adhabu yoyote kwa matamanio yake kwa kuwa Shari'ah imekataza baadhi ya adhabu kama kuadhibu kwa kuchoma moto n.k. Lakini baadhi ya hudood au jinayaat zinaweza kutekelezwa kama ta'zeer.

Ta'zeer ni tofauti na adhabu nyingine kwa sababu mtu anayehukumiwa na ta'zeer anaweza kusamehewa na Serikali au kifungo chake kikapunguza ilhali katika hudood au jinayaat hakuna msamaha kutoka kwa Serikali. Kwa sababu hudood au jinayaat zinapewa yule ambaye amekiuka haki ya Mwenyezi Mungu (swt) na wanadamu pia. Hivyo basi, uhalifu unaostahiki hudood au jinayaat unaadhibiwa bila mbadala. Lakini, uhalifu unaostahiki ta'zeer kama kumshutumu Khalifah amefanya makosa n.k Serikali inaweza kumpunguzia au hata kumsamehe muhalifu.

Hukumu ya ta'zeer inapatikana kupitia Qiyaas (mchakato wa kuvua hukumu ya kiShari'ah kwa kulinganisha) kwa mujibu wa hali ya uhalifu wenyewe. Khutuba kutoka kwa Mtungaji (swt) ameweka qareena (kielekezi) kuhusu ukubwa wa kitendo kibaya kwa mujibu wa adhabu inayotakiwa kuvuliwa.

Zaidi ya hayo, kutabbani na kutekeleza adhabu kama hizo zinatakiwa iwe kupitia kufahamu waqiah na kwa mujibu wa 'illah (sababu ya kiShari'ah) zinazohusiana na "kukinga (kutokana na haramu) kama alivyofunua Mwenyezi Mungu (swt), (وَلَكُمْ فِى ٱلْقِصَاصِ حَيَوٰةٌ) "Mtakuwa nao uhai mzuri katika kulipiza kisasi." (TMQ 2:179). Mifano michache ya ta'zeer ni kama:

1. Lau mtu atajaribu kubaka lakini kwa sababu ya kuweko na kizuizi asifikie kiwango cha kufanya ngono inayostahiki hadd, ataadhibiwa kwa ta'zeer ya kutiwa jela miaka mitatu pamoja na kupunguziwa idadi ya bakora na kuhamishwa. Hii ni kwa sababu itakuwa amefanya kitendo cha haramu kinachostahiki hadd lau kusingekuwepo na kizuizi na kwa kuwa kitendo kibaya hakikufikia kiwango cha hadd, muhalifu huadhibiwa kwa ta'zeer.
2. Kuuza fasihi chafu, video, audio na huduma zote zinazohusiana na hizo zinaadhibiwa kwa kutiwa jela miezi sita.
3. Lau mtu atakunywa kilevya kisichokuwa pombe, mfano hash au madawa, basi ataadhibiwa kwa bakora na kutiwa jela miaka mitano pamoja na faini.
4. Lau mtu ambaye anajua kuwa mali ni ya uwizi na akainunua vivyo hivyo, basi ataadhibiwa kwa kufungwa jela kifungo kati ya miezi miwili au miaka miwili pamoja na jukumu la kumlipa aliyeibiwa.
5. Lau mtu atakuwa na nia ya kushiriki katika kuuendea kinyume umoja wa Serikali ya Kiislamu, kwa kupigia debe asbiy'yah (ukabila), basi ataadhibiwa kwa kutiwa jela kwa mujibu wa ukubwa wa uhalifu alioutenda kwa muda wa kati ya miaka mitano na miaka hamsini.

4. Mukhalafaat

Shari'ah umeweka adhabu za Mukhalafah ambazo huadhibiwa wale waliokiuka hukumu (maagizo) ya Imamu (Khalifah). Kwa sababu Shari'ah imemruhusu Khalifah kutabbani sheria katika masuala ya mubah, mfano sheria za barabarani ambazo zinaingia katika idara ya Serikali kwa mujibu wa mashauriano na wajuzi au baraza la Ummah, ni muhimu kuwa ukiukwaji wa sheria hizo uwekewe adhabu. Kama kukiuka sheria za kiidara ni uasi kwa Imamu. Mfano kuwaasi mu'awineen (wasaidizi wa Khalifah) ni kumuasi Khalifah kwa kuwa Khalifah ndiye aliyewaagiza watekeleze maagizo ya sheria za Kiislamu. Mwenyezi Mungu (swt) amefaradhisha kumtwii Khalifah, kama Yeye (swt) alivyoagiza:

يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوٓا۟ أَطِيعُوا۟ ٱللَّهَ وَأَطِيعُوا۟ ٱلرَّسُولَ وَأُو۟لِى ٱلْأَمْرِ
"Enyi mlio amini! Mtiini Mwenyezi Mungu, na mtiini Mtume na wenye madaraka katika nyinyi." (TMQ 4:59), meaning listen and obey those who are granted authority by the Ummah.

Zaidi ya hayo, kumtwii Ameer ambaye amechaguliwa na Khalifah ni faradhi kwa Waislamu, kama alivyotufahamisha Rasulullah (saw),

من أطاعني فقد أطاع الله، ومن يعصني فقد عصى الله، ومن يطع الأمير فقد أطاعني، ومن يعص الأمير فقد عصاني
"Yeyote atakaye nifuata mimi, amemfuata Mwenyezi Mungu; na ambaye hatonifuata mimi, hamfuati Mwenyezi Mungu; na anaye mfuata Ameer (kiongozi), basi amenifuata mimi; na ambaye hamfuati Ameer, basi hanifuati mimi." (Bukhari / Muslim).

Lakini, kumfuata huko ni katika mema (ma'roof) pekee na sio katika maovu (munkar) kama alivyosema yeye (saw) «إِنَّمَا الطَّاعَةُ فِي الْمَعْرُوفِ» "Kufuata ni katika yaliyo mema pekee." (Sahih al-Bukhari 7145).

Ni ushahidi tosha kuwa kujifunga na maagizo ya Imamu ni sharti kwa yeye kutekeleza sheria za Kiislamu na sio sheria za Kikafiri. Hivyo basi, kutofuata maagizo ya Khalifah ni kosa (kukiuka) linastahiki adhabu kwa mujibu wa hukumu ya Qadhi wa Serikali ya Kiislamu. Baadhi ya mafuqahaa' (wanasheria wa Kiislamu) wamejumuisha mfano wa adhabu hizo ni ta'zeer na sio kama kifungu tofauti. Lakini, katika kupangilia wakatofautisha ta'zeer na mukhalfaat kuwa ta'zeer ni adhabu zinazopewa

***Endelea Uk..15***

wanao kiuka maamrisho ya Mwenyezi Mungu (swt) moja kwa moja na ilhali mukhalafaat ni adhabu zinazopewa wanao kiuka maagizo ya Khalifah.

Ni muhimu kufahamu kuwa maagizo yanayotolewa na Khalifah yanahusiana pekee na tabbani za ahkaam na sio utungaji wa ahkaam hizo kibinafsi kwa sababu ni haramu kwa Khalifah kutabbani chochote isipokuwa Shari'ah.

Ama kuhusu masuala ya mubah, mifano ya hatua za kiusalama wa bait ul-maal (Hazina ya Serikali), ujenzi wa miji na mipango ya jeshi n.k, haya huachiwa Khalifah kuamua kwa mujibu mashauriano. Hili limevuliwa kutokana na ufahamu wa hadith «أَنْتُمْ أَعْلَمُ بِأَمْرِ دُنْيَاكُمْ» "Munayo elimu bora zaidi (katika masuala ya kiufundi) katika dunia yenu." (Sahih Muslim 6128).

Ina maanisha masuala ya mubah yanahitaji elimu na ujuzi wa mambo ya kidunia na hivyo kuweza kutegemea akili na tajriba ya mwanadamu kuhusiana na waqiah unavyosonga. Kwa mfano huo, Khalifah atatabbani sheria zitakazo tatua masuala yanayo ingia katika idara na aweza kufunga adhabu katika ukiukaji wa maagizo yake ya kiidara.

**Imeandikwa kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na**

**Muhammad Sadiq Amin**

# Vipi Khilafah Itazuia Dhuluma za Kisiasa?

Demokrasia, uhuru wa rai na haki ya kumchagua na kumhisabu mtawala, ni miito inayo pigiwa debe chini ya serikali za kibinadamu zilizoko leo duniani, lakini, urongo wa miito hii hudhihirika pindi mtu binafsi au kikundi cha watu kinapozikashifu serikali hizi na ufisadi wao, au kinapodai haki ambayo wameipoteza au majukumu ambayo serikali hizi zimefeli kutimiza kwa watu wake. Magereza ya Urusi, mrithi wa Muungano wa Kisovieti, inayo sherehekea siku ya wahanga wa mateso ya kisiasa mnamo 3/10 kila mwaka, wakikumbuka mgomo wa njaa uliofanyika mnamo 30/10/1974 M na ulioanzishwa na wafungwa katika kambi za Mardovia na Perm, ambako wafungwa wa kisiasa walitangaza mgomo wa njaa wakilalamika dhidi ya mateso ya kisiasa yaliyotekelezwa na Muungano wa Kisovieti, magereza haya ni shahidi kwa hili, na magereza ya serikali za kihalifu katika ulimwengu wa Kiislamu, na wauwaji wake nchini Misri, Syria, Libya, Uzbekistan na biladi nyenginezo za Waislamu pia yanathibitisha hili.

Na kwa sababu Khilafah ni ndhamu kutoka kwa Mwenye hekima aliye Mjuzi wa kila kitu, na kwa sababu ndio suluhisho sahihi na sio tu badala kwa serikali hizi za kibinadamu, tutawasilisha katika makala haya mistari mipana inayozuia ukandamizaji na mateso ya kisiasa ambayo tunayashuhudia leo:

1- Dola ya Khilafah sio dola ya kiaskari inayokazanisha mshiko wake juu ya watu na kuwachunguza mienendeo yao, na kuweka kamera ili kuwachunguza sehemu za hadharani na wakati mwengine hata katika sehemu za faragha. Au kufuatilia simu zao au akaunti zao katika mitandao ya kielektroniki, kuwakamata na kuwatesa kwa sababu ya nukuu za tweet au chapisho katika tovuti hizi, au kuwaficha nyuma ya jua "kwa sababu ya mafungamano yao ya kisiasa" kama zifanyavyo serikali hizi katika ulimwengu wa Kiislamu leo. Uislamu umeharamisha kuwachunguza Waislamu kwa nasi ya Aya (وَلَا تَجَسَّسُوا) "Na wala musichunguze" [Al-Hujurat: 12]. Huu ni uharamu jumla wa kuchunguza na ni sharti uendelee kama wa jumla isipokuwa kuwe na dalili maalum. Hii imethibitishwa kupitia riwaya iliyo ripotiwa na Ahmad na Abu Dawud kwa silsila kutoka kwa Al-Miqdad na Abu Umamah pindi waliposema:

إِنَّ الأَمِيرَ إِذَا ابْتَغَى الرِّيبَةَ مِنَ النَّاسِ أَفْسَدَهُمْ "Wakati mtawala anapotaka kuweka uchunguzi dhidi ya watu, basi huwafisidi."

Hivyo basi, kuwachunguza Waislamu imeharamishwa. Hukumu hii pia inawahusu watu wa Dhimmah miongoni mwa raia wa Dola hii. Hivyo basi, uchunguzaji wa raia ni haramu, Waislamu na wasiokuwa Waislamu.
Uislamu pia ulimharamisha mtawala kuwatesa na kuwadhuru watu. Muslim amesimulia katika Sahih yake kutoka kwa Hisham ibn Hakim ibn Hizam, Amesema: Nimemsikia Mtume (saw), akisema: إِنَّ اللهَ يُعَذِّبُ الَّذِينَ يُعَذِّبُونَ النَّاسَ فِي الدُّنْيَا"Hakika Mwenyezi Mungu atawaadhibu wale ambao wanawaadhibu watu katika hii dunia".

Mtume (saw) pia amesema:

نْفَرَانِ مِنْ أَهْلِ النَّارِ لَمْ أَرَهُمَا، قَوْمٌ مَعَهُمْ سِياطٌ كَأَذْنَابِ الْبَقَرِ يَضْرِبُونَ بِهَا النَّاسَ...

"Watu aina mbili ni katika watu wa Motoni ambao sijapata kuwaona: watu walio na mijeledi mithili ya mikia ya ng'ombe, wanawapiga kwayo watu ..." (Imesimuliwa na Muslim). Uislamu pia umeharamisha kushambulia matukufu ya Waislamu, heshima zao, na mali zao na kukiuka faragha ya nyumba zao, Mtume (saw) amesema:

كُلُّ الْمُسْلِمِ عَلَى الْمُسْلِمِ حَرَامٌ دَمُهُ وَمَالُهُ وَعِرْضُهُ

"Imeharamishwa kwa Muislamu kumkiuka Muislamu katika damu yake, mali yake, na heshima yake".

2- Chini ya Khilafah, watu wana haki ya kuzungumza na

*Endelea Uk..16*

kutoa rai zao, na kuwahisabu watawala na kuwabadilisha endapo watawanyima raia haki, kushindwa kutimiza majukumu kwao, kupuuza mambo yao, kukiuka hukmu za Kiislamu au kuhukumu kwa hukmu zisizoteremshwa na Mwenyezi Mungu. Watu wana haki ya kufanya hivyo ima kibinafsi binafsi au kwa ujumla wao kupitia Baraza la Ummah au vyama vilivyoko ndani ya Dola. Mwenyezi Mungu (swt) amefanya kuamrisha mema (Ma'ruf) na kukataza maovu (Munkar) ni wajib juu ya Waislamu, Yeye (swt) amesema:

الَّذِينَ إِن مَّكَّنَّاهُمْ فِي الْأَرْضِ أَقَامُوا الصَّلَاةَ وَآتَوُا الزَّكَاةَ وَأَمَرُوا بِالْمَعْرُوفِ
وَنَهَوْا عَنِ الْمُنكَرِ

"Wale ambao tukiwapa madaraka katika nchi husimamisha Swala na wakatoa Zakah, na wakaamrisha mema, na wakakataza mabaya." [Al-Hajj: 41].

Na ziko Hadith zinazotaja kumhisabu mtawala haswa. Muslim amesimulia katika Sahih yake kutoka kwa Umm Salamah (ra) kuwa Mtume (saw) amesema:

سَتَكُونُ أُمَرَاءُ فَتَعْرِفُونَ وَتُنْكِرُونَ، فَمَنْ عَرَفَ بَرِئَ، وَمَنْ أَنْكَرَ سَلِمَ، وَلَكِنْ مَنْ
رَضِيَ وَتَابَعَ» قَالُوا: أَفَلا نُقَاتِلُهُمْ؟ قَالَ: لا، مَا صَلَّوْا

"Na kutakuweko na viongozi na mutawajua (matendo yao) na mutawachukia, basi mwenye kujua (matendo yao na kujaribu kuwazuia), ataepushwa mbali, na mwenye kuchukia atasalimika, lakini mwenye kuridhia na kufuata ameangamia". Wakauliza: 'Je, tuwapige vita?' Akasema: "Hapana, maadamu wanaswali" na swala hapa ni majazi ya kuhukumu kwa Uislamu.

Mtume (saw), amesisitiza kuwapiga vita watawala madhalimu, licha ya madhara ambayo yatatokea katika kufanya hivyo, hata kama itapelekea mauwaji, ambapo yeye (saw) amesema:

سَيِّدُ الشُّهَدَاءِ حَمْزَةُ بْنُ عَبْدِ الْمُطَّلِبِ وَرَجُلٌ قَامَ إِلَى إِمَامٍ جَائِرٍ فَأَمَرَهُ وَنَهَاهُ فَقَتَلَهُ

"Bwana wa Mashahidi ni Hamza bin Abdul Muttwalib, na mtu atakaye simama mbele ya kiongozi jeuri akamwamrisha na kumkataza kisha (mtawala huyo) akamuua."

Haya ni miongoni mwa maneno faswaha katika kubainisha Haki na kuvumilia madhara hadi kifo ili kuwahisabu watawala na kupambana dhidi ya watawala madhalimu.

Kuna dalili nyingi katika historia ya Waislamu kuhusu Waislamu kuwahisabu watawala na kuitisha haki zao pasi na kunyimwa na yeyote. Walimuhisabu Omar ibn al-Khattab, alipokuwa juu ya minbar, juu ya ugawanyaji wa nguo za Kiyemeni. Vile vile, Bilal na Az-Zubayr miongoni mwa wengineo, walipinga na kuzozana naye kwa sababu hakuigawanya ardhi ya Sawad nchini Iraq baada ya kufunguliwa kwake; alijadiliana na kuwashauri maswahaba hadi alipowakinaisha rai yake. Vile vile Ali (ra) alikataa rai ya Uthman (ra), aliyekuwa Kamanda wa waumini, ya kukamilisha Hajj na Umrah.

3- Chini ya Khilafah, Baraza la Ummah litakuwa linawawakilisha watu kikweli na madukuduku yao na sio kwa njia ya kuwahadaa. Litawawakilisha katika kutoa rai kwa niaba yao, likitoa malalamishi yao, na kumhisabu Khalifah na wale walio mamlakani. Waislamu na wasiokuwa Waislamu, wanaume na wanawake, wana haki ya kuwa wanachama wa Baraza hili, ambapo Kifungu cha 107 cha Katiba Kielelezo iliyo tayarishwa na Hizb ut Tahrir kinasema:
"Kila raia ambaye ni mtu mzima na mwenye akili timamu, ana haki ya kuwa mwanachama wa Baraza la Ummah au Baraza la Wilaya, awe mwanamume, mwanamke, Muislamu au asiyekuwa Muislamu; mwanachama asiyekuwa Muislamu amefungika na kutoa malalamishi kuhusiana na dhuluma ya watawala au utabikishaji mbaya wa hukumu za Kiislamu."

4- Chini ya Khilafah, idara ya mahakama haitakuwa ni chombo cha dhuluma na kukandamiza watu, kuwazuia kutokana na kutekeleza haki yao ya kimaumbile ya kuhisabu na kutoa rai, kuwazulia mashtaka ya urongo dhidi yao kwa sababu ya mafungamano yao ya kisiasa na kutoa hukumu za kidhuluma dhidi yao, kama ilivyotokea katika mauwaji ya kinyama ya vijana tisa kutoka Misri mnamo Jumatano asubuhi, 20 Februari 2019, kwa msingi wa kuungama kwao kutokana na kuteswa kwa stima. Badala yake, mahakama zitakuwa ni mwenge wa haki, uadilifu na kuregesha haki kwa wenyewe. Mtawala hatakuwa na kinga wala mfanyikazi yeyote ndani ya dola. Kutakuweko na mahakama maalum ya kusikiza kesi dhidi ya Khalifah au watu walio mamlakani, kwa jina, Mahakama ya Madhalim. Ambapo, Mahakama ya Madhalim inajukumu la "kutoa hukumu ya kisheria kwa njia ya kulazimisha kuhusiana na mzozo wowote utakao kuwepo kati ya raia na Khalifah au yeyote katika Magavana wake au wafanyikazi, au tofauti yoyote iliyoko kati ya Waislamu kuhusu tafsiri ya nasi yote ya kisheria kutumika ili kuhukumu kwazo na kutawala kwa mujibu wake." (Taasisi za Dola ndani ya Khilafah katika Utawala na Idara).

Katika historia ya Waislamu, Khalifah wa Waislamu aliketi pamoja na mmoja wa raia wake mbele ya mahakama na kadhi akatoa hukumu upande wa mpinzani na kumshutumu Khalifah. Kisa cha Omar bin al-Khattab pamoja na mtu aliyetaka kununua farasi kutoka kwake ni maarufu mno, kama kilivyo kisa cha kadhi aliyetoa hukumu yake akimtaka Omar bin Abdul Aziz kuliondoa jeshi lake kutoka katika ardhi waliyoifungua kwa sababu hawakuwalingania watu wake katika Uislamu kabla ya kupeleka majeshi hayo, na visa vyenginevyo ambavyo vyaweza kuregelewa.
5- Chini ya Khilafah, kuasisi vyama vya kisiasa ndani ya Dola hii si haramu, maadamu vitasimama kwa msingi wa Uislamu, na kuasisi vyama kama hivyo hakuhitaji idhini ya Dola. Kifungu cha 21 cha Katiba Kielelezo iliyo tayarishwa na Hizb ut Tahrir kinaeleza: "Waislamu wana haki ya kuasisi vyama vya kisiasa ili kuwahisabu watawala au kufikia utawala kupitia Ummah kwa sharti

*Endelea Uk..17*

kuwa msingi wake uwe ni Itikadi ya Kiislamu na kwamba hukumu vinavyo tabanni ziwe ni hukumu za Kisheria. Uundaji wa chama hauhitaji ruhusa yoyote. Kikundi chochote kitakachoundwa kwa msingi wa ukafiri ni haramu.” Dalili yake ni maneno ya Mwenyezi Mungu (swt):

وَلْتَكُنْ مِنْكُمْ أُمَّةٌ يَدْعُونَ إِلَى الْخَيْرِ وَيَأْمُرُونَ بِالْمَعْرُوفِ وَيَنْهَوْنَ عَنِ الْمُنْكَرِ
وَأُولَئِكَ هُمُ الْمُفْلِحُونَ

“Na kuwepo miongoni mwenu kikundi chenye kulingania kheri, na kuamrisha mema na kukataza maovu na hao ndio waliofaulu” [Al-i-Imaran:104].

Mtazamo wa kuitumia ayah hii kama dalili ya kuasisi vyama vya kisiasa ni kuwa Mwenyezi Mungu (swt) amewaamrisha Waislamu kuwa na kikundi kinachobeba Da’wah ya Uislamu miongoni mwao, na vile vile kuamrisha Ma’ruf na kukataza Munkar.

6- Chini ya Khilafah ubwana uko kwa Shariah na utawala uko kwa Ummah. Ummah humchagua mtawala wake na kumpa ahadi ya utiifu juu ya Kitabu cha Mwenyezi Mungu (swt) na Sunnah ya Mtume (saw) ili kutabikisha Shariah. Mtawala huyo halazimishwi juu yao kutabikisha matakwa ya mabwana zake, kama ilivyo hali leo katika biladi za Waislamu. Dola ya Khilafah ina uwezo wa kisiasa wa kihakika, na hutekeleza siasa kwa sura yake halisi; kuchunga mambo ya watu, na sio kuwatawala juu ya shingo zao na kuwagandamiza na kuwadhulumu. Na chini ya Khilafah, mtawala na raia hufuata hukumu za Shariah na utiifu wa raia kwa mtawala ni sharti juu ya kushikamana kwake na hukumu za Shariah:

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا أَطِيعُوا اللَّهَ وَأَطِيعُوا الرَّسُولَ وَأُولِي الْأَمْرِ مِنكُمْ فَإِن تَنَازَعْتُمْ
فِي شَيْءٍ فَرُدُّوهُ إِلَى اللَّهِ وَالرَّسُولِ إِن كُنتُمْ تُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ ذَٰلِكَ خَيْرٌ
وَأَحْسَنُ تَأْوِيلاً

“Enyi mulio amini, mtiini Mwenyezi Mungu, na mtiini Mtume na walio na mamlaka miongoni mwenu. Na mutakapozozana katika jambo basi lirudisheni kwa Mwenyezi Mungu na Mtume, ikiwa kweli muna muamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho. Hayo ndiyo bora na ndiyo yenye mwisho mwema.” [An-Nisa: 59]

Kwa kutamatisha, nitarudi kwa lile nililo anza nalo, kutaja tena kuwa Khilafah Rashidah kwa njia ya Utume ndio suluhisho sahihi kwa matatizo ya Ummah huu, bali, kwa wanadamu wote. Ni nidhamu ya kipekee kutoka kwa Mwenye hekima aliye Mjuzi wa vitu vyote. Je, haijatosha miaka 98 ya dhuluma, unyanyasaji na mateso bila ya Khilafah?! Je, hatupaswi kuimarisha kujitolea kwetu na kuharakisha kuisimamisha?!

**Imeandikwa kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na**

**Bara’ah Manasrah**

# Talaka ni Halali Hata Kama ni Halali Inayo Chukiwa Zaidi

Kwa kuwa ni sheria kamili, imemsimamia mwanadamu na kumpatia njia za kumuwezesha kukidhi mahitaji yake ya kiviungo na kighariza pasina na kumsababishia majonzi yeye na wanadamu wengine. Na kuweka suluhisho mwanana na zilizo kamilika kwa matatizo na mazito yote anayo kumbana nayo. Huu ni Uislamu, Dini ambayo Muumba ameiidhinisha kwa watumwa Wake ili waweze kuishi kwa kufurahi, kutosheka na kutaka radhi za Mwenyezi Mungu wao. Kama ghariza nyingine, Uislamu unaangazia ghariza ya kuendeleza kizazi na kuhifadhi wanadamu na kuashiria njia halali ya kufikia hilo. Kwa hivyo ikatambua ndoa kuwa ni mahusiano matukufu baina ya wanandoa. Fungamano lenye nguvu linalo waunganisha, Mwenyezi Mungu asema:

وَكَيْفَ تَأْخُذُونَهُ وَقَدْ أفضى بَعْضُكُمْ إلى بَعْضٍ وَأَخَذْنَ مِنكُم مِّيثَاقاً غَلِيظاً

“Na mtachukuaje na ilhali mmekwisha ingiliana nyinyi kwa nyinyi, na wao wanawake wamechukua kwenu ahadi iliyo madhubuti?” [An-Nisa: 21]

Fungamano hili ambalo kila mmoja anayemuani Mwenyezi Mungu anatakiwa kujifunga nalo na asifuate suluhisho nyingine ambazo zinakidhi ghariza hii. Na ndio maana Uislamu ukatuamrisha sisi kufanya chaguo zuri na kusisitiza kuhusu wanaume wema wawe ni kwa wanawake wema:

وَالطَّيِّبُونَ لِلطَّيِّبَاتِ

“Na wanawake wema ni wa wanaume wema” [An-Noor: 26] Kwa hivyo mahusiano haya ni dhabiti, yenye kudumu katika maisha yao.

Lakini makosa yaweza kutokea katika kuchagua ima kwa kuchagua mume au mke, ambapo inapelekea kuharibu mahusiano baina yao na kutafuta maisha inakuwa vigumu kutokana na wao kuwa na tabia tofauti au kwa sababu ya mgongano katika maslahi yao, au kukosekana kwa utulivu na mapenzi kati yao. Natija yake ni kuwa maisha yanakuwa moto usiovumilika na suluhisho lisiloepukika hujitokeza: talaka! Naam, Uislamu umeweka sheria ya talaka na kuifanya kuwa ni halali inayo chukiwa zaidi –lakini ni suluhisho la dharura katika baadhi ya hali za ndoa ambapo hakuna makubaliano baina ya pande mbili kutokana na kuwa haiwezikani kuendelea kuishi pamoja.

Ili kuihifadhi chembe chembe hii kutokana na maangamivu hatari juu yake na kwa mujtama mzima, Uislamu umeweka sheria ya talaka. Na ili kuweza kutochafua mahusiano na kutoharibu fungamano madhubuti kwa kukosekana utulivu na makubaliano baina ya wanandoa, Uislamu ukaweka talaka. Kwa sababu Mwenyezi Mungu Anajua alivyoviumba na Anajua alivyoviweka ndani ya alivyoviumba. Mwenyezi Mungu akawahalalishia wanandoa njia ya kulifungua (kutoka katika) fungamano hilo ili wasielekee katika njia ambazo zitawapelekea kuyakiuka mahusiano yao na kumkasirisha Mwenyezi Mungu wao.

Ukristo ulipoliangazia suala hili, ili liona kuwa halikubaliki na haukuwaruhusu wanandoa kutalikiana (kuachana), kwa kuwa inalitizama kuwa ni fungamano tukufu. Mwanamume lazima aunganishwe na mwanamke mmoja kwa maisha yake yote na wanandoa lazima wawe waaminifu kwa viapo vyao vya ndoa tukufu. Kwa msingi huo ikaharamisha talaka kama sheria. Lakini ukajipata mbele ya hali ambayo wanandoa hawawezi kuishi pamoja na kuwasukuma kutafuta njia nyingine za kuishi, kila mmoja akikidhi matamanio na mahitaji yake anavyotaka. Hivyo basi, mahusiano haramu yakaanza kusambaa, mahusiano ya kifamilia kuvunjika na mujtama kuwa fisadi. Kanisa linategemea marudio yake ya kwanza, “kitabu Kitukufu” ambacho kinasema kwamba “mwanamume yeyote anayemuacha (kumpa talaka) mkewe, isipokuwa kwa makosa ya ya zinaa, ana msababishia mkewe kufanya zinaa, na yeyote anayeoa mwanamke aliyeachwa (kupewa talaka) anafanya uzinifu.” Lakini kutokana na ugumu uliokumbana nao katika kutoa uamuzi juu ya mahusiano ya ndoa zilizo na matatizo. Ili lazimishwa kutunga sheria ili kuruhusu talaka. Hii ikijumuisha kufanya uzinifu kati ya mmoja wa wahusika, kukiuka utukufu wa ndoa, uwenda wazimu kati ya mmoja wa wahusika na maumivu ya kihisia ambayo hayawezi kutibika na ambayo yamekuwa ni tishio hatari kwa maisha ya ndoa na kwa watoto, au mwanandoa ameondoka katika nyumba ya ndoa bila ruhusa au kumjuza mwenziwe na kwa muda wa takribani miaka mitatu au zaidi, na pia wakati ambapo mmoja kati ya wahusika aliingia katika ndoa kwa kulazimishwa na bila ya idhini yake au kuridhia.

Huo ndio msimamo wa Kanisa ambao unaitizama ndoa kuwa ni fungamano tukufu ambalo lazima lidumu na lisivunjwe. Lakini hata hivyo, baada ya kukumbana na changamoto katika familia nyingi ambazo zilihusiana na matatizo kati ya wanandoa, ikaruhusu matukio mengi ya kuachana (kupeana talaka).

Msimamo mwingine unaopigiwa debe ni ule wa uhuru na ukombozi wa mwanamke, unaolingania kuishi bila fungamano hilo. Hivyo basi, kila mmoja anaishi anavyotaka! Msimamo ambao wanaoshikilia wanalenga kuikandamiza familia na kuivunjilia mbali.

Muandishi maarufu, Simon de Beauvoir, anaitizama ndoa kuwa ni, “gereza la milele kwa mwanamke ambalo linakata matumaini yake na ndoto zake.” Anaitizama taasisi ya ndoa kama taasisi ya ukandamizaji wa

*Endelea Uk..19*

wanawake inayotakiwa kuvunjwa na kupigwa marufuku. Filosofia ya ukombozi wa wanawake pia nayo inapigia debe “uhuru wa mafungamano na uhuru wa kutengana wakati wowote kati ya watu wawili; ima wawe ni wa mahusiano ya jinsia moja au jinsia tofauti.” Imeleta fujo na mkorogo katika maisha, mchanganyiko wa kizazi na kuvunja familia na mujtama jumla.

Uislamu ni sheria ya Mwenyezi Mungu ambayo ni kitu bora cha kupangilia maisha ya mwanadamu. Nani anayejua kuhusu viumbe isipokuwa Muumba, na nani mbora wa kupangilia maisha yao na vitendo vyao kama si Yeye? Yeye amewawekea sheria ya ndoa ili kukidhi ghariza zao na kuendeleza kizazi na kuendelea kuzaana ili kizazi kiendelee kuwepo na maisha yao yaendelee. Na Yeye akawashajiisha wafanye chaguo zuri ili kuendeleza ndoa na kuishi katika maisha ya maelewano na utulivu. Lakini ukuruba wa mahusiano unaweza kuvurugwa na kazi za Shetani ili kuwatofautisha wanandoa, kisha kujigamba na kufurahia kufaulu hilo. Mtume (saw) alisema:

**إنّ إبليس يضع عرشه على الماء ثمّ يبعث سراياه فأدناهم منه منزلة أعظمهم فتنة يجيء أحدهم فيقول فعلت كذا وكذا فيقول ما صنعت شيئا قال ثمّ يجيء أحدهم فيقول: ما تركته حتّى فرّقت بينه وبين امرأته قال فيدنيه منه ويقول: نِعم أنت...**

Iblis huweka kiti chake juu ya maji; kisha akaitisha vikosi vyake vya kusababisha kukosekana maelewano; kilichoko karibu kwa cheo ni kile maarufu kwa kuleta mfarakano. Mmoja wao anakuja na kusema: “Nimefanya hili na hili.” Na husema: “Hujafanya kitu.” Kisha mwengine miongoni mwao anakuja na kusema: “Sikuwacha lolote mpaka nimeleta mfarakano baina ya mume na mkewe.” Basi Shetani humuendea karibu na kumwambia: “Umefanya vyema zaidi”

Ni kazi ya Shetani. Na licha ya kuwa ni jambo lililoruhusiwa na linalochukiwa na Mwenyezi Mungu, linabakia kuwa ni halali na suluhisho baada ya majaribio yote kufeli kutatua mizozo na tofauti zilizopo na maisha baina ya wanandoa kuwa magumu. Kwa hiyo, kuivunja ndoa linakuwa ni jambo muhimu na linakuwa ni suluhisho bora kutokana na maisha baina ya wanandoa kuwa mabaya zaidi ya kuvunjwa huko.

Uislamu ulikuja na kuusafisha mujtama na machafu yote, fikra fisidifu na mahusiano ya kimakosa na kumakinisha usafi na utulivu kwa mujibu wa fikra na mahusiano yake na hivyo kukawa kusafi. Hizo ni fahamu, tiba na suluhisho zake kwa mahusiano ya wanandoa pale ambapo imefikia kuwa maisha ni vigumu kuendelea na hivyo talaka ndio njia pekee ya kutatua suala hilo kwa kuwa mahusiano yamekosa utulivu, mapenzi na kuhurumiana na badala yake ni chuki, uadui na kukosekana kwa maelewano. Mwenyezi Mungu (swt) amelizungumzia suala hilo kwa ukamilifu katika Surah, At-Talaq (Talaka) na akaiweka wazi kwa mapana ndani ya Surat al-Baqarah. Hivyo basi, hukumu Yake kuhusiana nayo (talaka) imeelezewa na kufafanuliwa kwa watu ili waweze kupeleka maisha yao kwa mujibu wa (hukumu) hizo kama anavyotaka Mwenyezi Mungu ili kuhifadhi mujtama, ambao lau chembe chembe yake moja itaingia maradhi, utasimama madhubuti ili kuhimili mashambulizi hayo na kuyashinda. Hakika, ndani ya Dini hii tukufu zimo suluhisho ambazo kupitia kwazo mujtama waweza kujikinga na madhara na kumakinisha misingi yake. Katika Uislamu, zimo kheri zote licha ya kwamba kwa mujibu wa mitizamo yetu tunaona kuwa labda hatuna manufaa au kuna uovu katika vitu au athari mbaya au mapungufu kutokana na hukumu zetu za (kiakili), kwa kuwa hatuoni siri zake na Mwenyezi Mungu pekee ndiye anayejua:


**وَعَسَىٰ أَن تَكْرَهُوا شَيْئًا وَهُوَ خَيْرٌ لَّكُمْ وَعَسَىٰ أَن تُحِبُّوا شَيْئًا وَهُوَ شَرٌّ لَّكُمْ وَاللَّهُ يَعْلَمُ وَأَنتُمْ لَا تَعْلَمُونَ**

“Lakini huenda mkachukia kitu nacho ni kheri kwenu. Na huenda mkapenda kitu nacho ni shari kwenu. Na Mwenyezi Mungu anajua na nyinyi hamjui.” [Al-Baqara: 216]

Talaka hata kama itaoneka ina ubaya ndani yake; ni nzuri kwa idhini ya Mwenyezi Mungu kwa wanandoa, watoto na familia kwa ujumla. Ni bora kuliko wao kuishi pamoja –baada ya kuwa haiwezikani –kwani maisha hubadilika na kuwa moto na kuleta maovu na kukandamizana. Ndoa ni fungamano la ukaribu na madhubuti ambalo Uislamu umesisitiza lijengwe kwa nguzo madhubuti ambazo zitaweza kuhimili matatizo na tofauti watakazo kumbana nazo wanandoa na kuzitibu kwa mujibu wa vipengee walivyo tabbani na kwa mahusiano baina yao ambayo yamesimama juu ya mapenzi ya Mwenyezi Mungu na kufanya kazi kumridhisha Yeye. Hili ndilo ambalo Mwenyezi Mungu ameliamrisha kwa watumwa Wake ili familia iweze kuwa na maelewano, kuhurumiana na mapenzi. Mujtama unakuwa na uwiano na kufungamanisha wanachama wake kuwa na mashindano ya kutafuta kheri na radhi za Bwana wa Mbingu na Ardhi. Na lau mahusiano haya yatakumbwa na matatizo na mapungufu basi suluhisho zipo ambazo zimeelezewa na sheria ya Ar-Rahman.

**Imeandikwa kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na**

**Zaina Al-Saamit**



# Njia ya Mtume (saw) Kuleta Mageuzi

## Halaqa 22: Jihad

Katika halaqa hii tutazungumzia JIHAD ambayo ni ذروة سنام الإسلام (Nundu ya Uislamu) hii ni kinaya ya utukufu wa Jihad na nafasi yake ya juu katika Uislamu.

Kupitia Jihad Uislamu na Waislamu wanapata izza, ukafiri na ushirikina kupata udhalili, na kuipitia Jihad Dola ya Kiislamu hupata hifadhi na kubakia tukufu yenye himaya. Kuipitia JIHAD huhifadhiwa haki na kurudishiwa wenyewe, na kwayo huchungwa heshima ya Waislamu, Matukufu yao, cheo chao, Ardhi zao na majumba yao. Na kwa Jihad huhifadhiwa Uislamu jumla.

Na Dola ya Kiislamu inatabikisha Uislamu juu ya Waislamu na kubeba Risala yake kwa ulimwengu kwa njia ya Jihad. Watu wanapoiwacha Jihad wanadhalilika mbele ya maadui zao.

Jihad ndiyo ambayo wema walio tangulia walikuwa na pupa juu yake kiasi wakapigana Jihad kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na kuipa haki Jihad mpaka ikawafikia yakini (kifo). Walitafuta kifo wakapewa maisha, wakafuzu kwa furaha ya nyumba mbili "Dunia na Akhera" wakapata kufaulu na daraja za juu katika Jannah ya milele ambayo Mwenyezi Mungu amewaandalia waja wake waumini.

Na kwa hakika inasikitisha sana na kutia uchungu kwa Waislamu wote wa Mashariki ya Ardhi na Magharibi yake, iwe maudhui yanayohusu masuala nyeti ambayo kwayo Waislamu na Uislamu utapata izza yanabakia kusomeshwa kinadharia, na inakuwa kuzungumziwa kwake ni mujarad wa maneno tu na khutba zinazotolewa juu ya maminbar, wakati sisi tunahaja sana kuyaona katika uhalisia na kuyahisi yanatabikishwa utabikishaji wa kivitendo katika maisha ya Waislamu.

Wallahi nafsi zetu zimechoshwa na udhalili, Wallahi nafsi zetu zinatamani Jannah ya milele ambayo Mwenyezi Mungu amewaandalia MUJAHIDINA.

Na ili tuvue mavazi ya udhalili kutoka katika nafsi zetu, na tufaulu kwa kupata radhi za Mola wetu, hatuna budi ila kufuata njia aliyotuchorea Mtume wetu na KIONGOZI wetu صلى الله عليه وسلم na tufanye kazi kwa bidii na ikhlasi, katika kubeba Da'wah,

Na tusubiri na kutaraji kwa Mwenyezi Mungu nusra yake na msaada wake kwa hiki kikundi kilicho amini imani ya yakini na iliokatikiwa kuwa Nusra inatoka kwa Mwenyezi Mungu peke yake.

Hiki kikundi ambacho hakitambui uchovu wala kukata tamaa, bali kitabakia kinafanya kazi na kufanya kazi, na kubisha milango iliyofungwa mpaka ifunguliwe kwa idhni ya Mwenyezi Mungu.

Tunamuomba Mwenyezi Mungu (swt) wakati huo uwe karibu, na kwa mikono yetu, hakika yeye ni mwenye kusikia aliye karibu mwenye kukubali dua.

Mshairi asema:

أخلق بذي الصبر أن يحظى بحاجته

Kuwa na tabia ya mwenye subra anaye subiri mpaka haja yake ikidhiwe

ومدمن القرع للأبواب أن يلجا

Na anaye dumu kubisha milango mpaka aingie



Email: info@uqab.or.ke